# Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumapili Oktoba 20, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0581835
JUMAPILI
www.ippmedia.com
0745 700710 LIKE & FOLLOW US
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com




**MESSI UWANJANI KLABU BINGWA YA DUNIA 2025**
UKURASA 21

UKURASA WA 2
**Mkuu** kituo polisi ampiga, na kumvunja raia mkono

UKURASA WA 7
**Waziri** Masauni ashangaa magari polisi kuchakaa kwa muda mfupi




UKURASA WA 11
MAISHA
**Akikwambia** nimemwacha mke nitakuoa, jitafakari

## RIPOTI MAALUM

# Watoto walivyogeuka kitegauchumi mitaani

• **Watumika** kuchangisha fedha za makanisa na misikiti, wazazi, viongozi wa dini wang'aka... *Endelea ukurasa 2*



UKURASA 24
**YANGA MOTO ULEULE DHIDI YA SIMBA**

## Ajali ya magari matatu ilivyoua 14, kujeruhi 12
UKURASA 2




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akijiandikisha kwenye Daftari la Wapigakura, kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mtaa, Vijiji na Vitongoji katika kituo cha Shule ya Msingi Nandagala, kitongoji cha Nanguruwe, Kata ya Nandagala, Ruangwa, mkoani Lindi jana. Kushoto ni Ofisa Uandikishaji, Alexander Mmole. **Habari Uk. 5. PICHA: OWMJUMA**



# Gambo amtuhumu Lema kuvuruga uandikishaji
UKURASA 2

**MICHEZO** NGORONGORO HEROES YAIPANIA KENYA UK.23 KATUNI UK.6

# Adaiwa kumuua babaye kwa kumkaba shingo

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MENGI yameibuka baada ya kifo cha aliyekuwa Msajili wa Vyama vya Michezo Tanzania, Riziki Majala (54), mkazi wa Kibondeni, Kwamatiasi, Kibaha, mkoani Pwani anayedaiwa kuuawa na mwanawe kwa kukabwa shingo.

Mtoto wa marehemu, Abdulkarim Riziki, akizungumza na mwandishi wa habari hii mjini hapa jana, alisema siku moja kabla ya kifo cha baba yake alishinda naye wakijadili mambo mbalimbali kuhusiana na uhamisho wake kutoka Baraza la Michezo kwenda Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Riziki alisema baada ya kumalizana na baba yake, alirudi Dar es Salaam ambako anaishi na ilipofika asubuhi, alipokea simu nyingi akielezwa kuhusiana na msiba wa baba yake, anayedaiwa kuuawa na kaka yake, anayefahamika kwa jina la Juma Riziki.

"Nilipofika (Kibaha) nilishuhudia kaka yangu amechukuliwa na polisi kwa mahojiano. Kaka yangu ni mtu wa sigara na pombe, mara nyingi tuhuma hizo za wizi na ukabaji zimekuwa zikiletwa nyumbani na wahusika.

"Pale nyumbani alikuwapo mama yetu mdogo, lakini naye aliondoka baada ya kushindwa kukaa pamoja na kaka kutokana na tabia zake," alidai.

Ndugu wa marehemu, Ben Ngozi, alisema taarifa za msiba wa baba yake mdogo alizipata kuwa amekutwa ameuwawa nyumbani kwake kwa madai ya kukabwa shingo na mwanawe.

Mpwa wa marehemu, Zuwena Seif, alisema mara ya mwisho kuzungumza na Majala ni usiku wa tukio hilo alipompigia kujadili mustakabali wa kesi yake ya mirathi ambayo (Majala) alikuwa wakili wake. "Oktoba 17, mwaka huu, niliongea na mjomba saa tatu usiku nikamsikia Juma anaomba fedha ili aende Bukene, Tabora aliko mama yake mzazi, nikamwambia mpe simu niongee naye nimtumie hiyo fedha, Juma akajibu 'sitaki kuongea na simu na mtu, mzee ninaomba fedha' ndipo mjomba akakata simu," alisema.

Alisema juzi alikuta simu imepigwa kwa namba ya marehemu na alipoipiga ilikuwa inatumika na alipotuma ujumbe haukujibiwa na alipopiga tena alipokea mtuhumiwa ambaye alimjulisha kuhusu kifo hicho.

"Nilimwuliza imekuwaje akasema, alitoka juzi (Oktoba 17) usiku kwenda baa ambayo inajulikana kwa jina la The Game Kwa Mathias na kwamba, aliporejea usiku alipofungua mlango ukawa mzito, alipousukuma akakuta baba yake amefariki dunia.

"Niliwapigia ndugu zangu wanaoishi maeneo jirani na kwa mjomba nikawaambia waende kuhakikisha na walipofika wakanieleza hali halisi, ndipo nikawaomba waende polisi," alisema Zuwena.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kibondeni, Kata ya Mkuza, Issa Sama, alisema alipokea taarifa za tukio hilo juzi kutoka kwa balozi ambaye alimweleza kuhusiana na tukio hilo na baada ya kufika alikuta watu wengi.

"Huyu Juma katika mtaa wetu ana historia ambayo si nzuri. Ni mmoja wa vijana wenye matukio ya kujirudiarudia kukaba kwa kutumia visu. Mara nyingi anakamatwa anatoka kwa dhamana na anaachiwa baada ya walalamikaji kutokwenda kufuatilia.

"Hata Majala tulimweleza kuhusiana na tatizo la kijana wake na jana kwa taarifa ni kwamba, alimwomba baba yake fedha Sh. 20,000 kuwa anataka kusafiri.

"Baba yake akamwambia hana, kwa taarifa za majirani walisikia usiku ugomvi baba akitoa sauti kulalamika kuwa Juma anamuua hawakutoa taarifa kwakuwa mara kwa mara kulikuwa na ugomvi katika nyumba hiyo," alisimulia mwenyekiti huyo.

Sama alisema walishuhudia sehemu ulikolala mwili kuna damu na eneo la shingoni kumevimba kama amekabwa, huku mgongoni kukiwa na alama za mchubuko.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Muhudhwari Msuya, alidhibitisha mtuhumiwa huyo kushikiliwa na Jeshi la Polisi na kwamba amekiri kuhusika na mauaji hayo.

Kaimu Msajili wa Vyama vya Michezo Nchini, Evordy Kyando, alisema wamepoteza mtaalamu wa michezo ambaye alikuwa mwalimu mzuri asiyechoka kuelekeza watu pale ushauri wake ulipohitajika.

Amewahi kuwa mwalimu katika Shule ya Sekondari ya Wavulana Kibaha, Katibu wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Pwani (COREFA) na kuwa katika vyama vingine vya michezo kabla ya kuwa Msajili wa Vyama vya Michezo, nafasi ambayo aliondoka Juni, 2023 na kupangiwa majukumu mengine kabla ya kuhamishiwa Wizara ya Elimu hivi karibuni.



Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Masauni na Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillus Wambura, wakiwa kwenye moja ya magari 77 aina ya GWM P Series Double Cabin, yaliyokabidhiwa kwa wizara hiyo na Kampuni ya Kifaru Motor Ltd, Dar es Salaam jana, ikiwa ni mwendelezo wa utekelezaji wa mkataba kati yake na Kampuni ya Ashok Leyland ya nchini India. Habari Uk. 7. **PICHA: ROMANA MALLYA**

# Gambo amtuhumu Lema kuvuruga uandikishaji

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MBUNGE wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo, amedai Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema, amekodisha magari mawili aina ya Toyota Spacio na Toyota RAV 4, ili kufanya vurugu katika mchakato wa uandikishaji wa Daftari la Wakazi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, Gambo alidai anaujua mpango wa Lema wa kukodi magari na kubeba wanafunzi kuwazungusha katika vituo vya uandikishaji, kwa ajili ya uchaguzi unaokuja.

"Ndugu yangu Lema mpango wake wa kukodi gari na kuwabeba wanafunzi kuwazungusha katika vituo vya kujiandikisha, kwa ajili ya uchaguzi ujao na wanafunzi ambao hawajatimiza umri wa kupiga kura, wakiwamo wenye umri wa miaka 15 hadi 18, tunaujua.

"Na video tunazo sema tu hatutaki kutoa, kwa sababu tutakosa kupata taarifa nyingine za mipango wanayoendelea nayo," alisema.

Gambo alidai kuwa pamoja na Lema kupiga kampeni watu kujiandikisha, anashangazwa na kitendo chake cha kuonekana akijiandikisha juzi, jambo ambalo anasema sio sawa kwa kiongozi kusubiri nyakati za mwisho kwenda kujiandikisha.

"Tulitumia ushawishi mkubwa kumtaka Lema akajiandikishe, ilibidi nimtumie shangazi yangu (Mke wa Lema), ili amshawishi kwenda kujiandikisha na kwa kuwa ni watu wawili tu wenye kusikilizwa na Lema yaani Freeman Mbowe na Neema mke wake.

"Nimpongeze shangazi yangu kwa kufanikiwa kumshawishi hadi akaenda kujiandikisha na kuweza kutupia picha katika ukurasa wake wa Instagram," alidai Gambo.

Alisema Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimejitosheleza, hivyo hakiwezi kufanya mambo yanayotuhumiwa na CHADEMA kuwa wanaandikisha wapigakura wasiokuwa na vigezo, ikiwamo kuwaandikisha wanafunzi ambao hawana umri unaohitajika.

Alisema walidai kuwa majina yanatumwa kwa njia ya mitandao ya kijamii, kwa ajili ya kuandikwa katika Daftari la Wakazi.

Nipashe ilipomtafuta Lema kwa njia ya simu kujibu tuhuma hizo, alisema hana cha kijibu na hawezi kuzungumzia jambo hilo.

Katibu wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini, Amani Golugwa, alipopigiwa simu kujibu hoja hizo za Mbunge Gambo kutuhumu kuwapo kwa magari mawili yanayotumika kuleta vurugu katika mchakato huo, alikanusha madai hayo.

Alisema kama ni kweli Gambo ameona magari hayo, anatakiwa kuyakamata kuyapeleka Kituo cha Polisi, ili sheria ichukue mkondo wake.

"Kwa kifupi tu niseme, Gambo anatafuta kujibiwa na Lema, lakini hawezi kumzungumzia maana hana madhara yoyote kwake.

"Ameona Lema hamzungumzii popote, hivyo anaamua kutafuta aanze kumzungumzia na kuhusu hayo magari anayosema kama ana uhakika ameyaona ayakamate ayapeleke polisi, ili sheria iweze kuchukua mkondo wake.

"Kwa nini anazungumza na nyinyi waandishi wa habari na wakati Jeshi la Polisi lipo. Kwanini asiwaeleze," alisema Golugwa.

# Mkuu kituo cha polisi ampiga, kumvunja mwananchi mkono

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Makete, mkoani Njombe, anadaiwa kumkamata mwananchi, Levis Mahenge, kumpeleka Kituo cha Polisi na kumpiga hadi kumvunja mkono. Kutokana na tukio hilo, Jeshi la Polisi nchini kupitia Msemaji wake, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP) David Misime, katika taarifa yake jana, alieleza hatua ambazo zimeshachukuliwa dhidi ya kiongozi huyo.

"Ufafanuzi ni kwamba, tukio hilo lilitokea Oktoba 9, mwaka huu, saa 12:30 jioni. Baada ya tukio hili kugundulika na uongozi wa Polisi Mkoa wa Njombe, jalada lilifunguliwa na ushahidi ukakusanywa na uchunguzi umekamilika.

"Hivi sasa hatua za kinidhamu zinaendelea kukamilishwa dhidi ya mkuu wa kituo hicho na baada ya hatua hizo, kwa sababu tuhuma zinazomkabili ni za kijinai zitafuata," alisema.

HABARI KITAIFA

# Mwinyi ataka waumini kujitathmini kimatendo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka waumini wa dini ya Kiislamu, kujitathmini na kujua umuhimu wa Ibada kwenye matendo yao ya kila siku.

Dk. Mwinyi alisema hayo alipotoa salamu kwa waumini hao, baada kujumuika nao kwenye ibada ya sala ya Ijumaa, Msikiti wa Muhammad Ali, Kidongo Chekundu, mkoa wa Mjini Magharibi.

Alisema ni wajibu wa kila muumini kuitathmini nafsi yake na anaowaongoza, ili kubaini kiasi gani maisha yao yanalingana na ibada wanazozitekeleza kila siku.

Alisema kuna mambo mengi yanaendelea ndani ya jamii, kwa sababu ya watu kukosa ucha Mungu.

Dk. Mwinyi alitaja baadhi ya mambo hayo kuwa ni pamoja na udhalilishaji, ubakaji na wizi.

Aidha, aliwahimiza waumini hao kufanya ibada, kwa kuwa ndiyo sababu kuu ya kuumbwa kwao.

Akitoa salamu, Katibu Mtendaji wa Ofisi ya Muft wa Zanzibar, Sheikh Khalid Ali Mfaume, aliwasisitiza viongozi kuwa mfano bora kwa watu wanaowaongoza, kwa kutenda mambo mema.

Sheikh Khalid aliwasisitiza vijana kuacha kushawishika na kujiunga na makundi maovu kwa kisingizio cha dini, badala yake kusimamisha sala kwa kuchunga wakati na nidhamu.



Baadhi ya mafundi wanaoboresha Barabara ya Morogoro, wakiondoa mbao kwenye ukuta uliojengwa, ili kuzuia mmomonyo wa ardhi eneo la Kimara Resort, Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Ajali magari matatu ilivyoua watu 14, kujeruhi wengine 12

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WATU 14 wamefariki dunia na wengine 12 kujeruhiwa katika ajali iliyohusisha magari matatu, likiwamo lori na costa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama ya Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alisema ajali hiyo ilitokea usiku wa kuamkia jana katika eneo la Kikavu, wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro.

Alisema lori aina ya FAW lenye namba T 517 EAE na tela namba T 287 CYF liligonga kwa nyuma gari T 553 aina ya Toyota Hilux na kisha kupoteza mwelekeo na kwenda kugongana uso kwa uso na gari aina ya Costa T 525 DKP.

Babu ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, alisema wakati huo, Toyota Coaster ilikuwa ikitokea Moshi mjini kwenda Arusha.

Alisema katika ajali hiyo, watu sita walifariki dunia papo hapo na wengine wanane walifariki dunia njiani wakipelekwa hospitalini.

Kwa mujibu wa Babu, majeruhi wa ajali hiyo wamelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Hai, Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC na Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mawenzi.

"Tunasikitika sana kupoteza nguvu kazi ya watu 14 ambao walikuwa wanakwenda katika shughuli zao na nitumie nafasi hii kutoa pole kwa ndugu wote waliopoteza wapendwa wao, lakini tuzidi kuwaombea majeruhi wote wapone haraka na kuendelea na shughuli zao," alisema Babu.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi, ili kubaini chanzo cha ajali hiyo, huku akitoa wito kwa madereva kuwa makini wanapoendesha vyombo vya vya moto hasa nyakati za usiku.

"Kama mnavyotambua barabara zetu ni nyembamba sana, maeneo haya yanaruhusu gari moja kupita na sio kupishana hivyo, niwaombe chukueni tahadhari sana mnapokuwa barabarani," aliagiza Babu.

Baadhi ya majeruhi akiwamo, Tunu Hassan, ambaye amelazwa hospitali ya Mawenzi, aliiomba serikali kuendelea kudhibiti madereva walevi, ili kupunguza ajali zinazozuilika.

"Sijui nini kimetokea ila niliona gari linakuja mbele yetu na ghafla nimejikuta hospitalini. Niiombe serikali ifanye jambo hasa katika upanuzi wa barabara katika eneo la Kikavu," alisema majeruhi mwingine, Happy Ngowi.

Msemaji wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mawenzi, Vena Karia, alisema wamepokea majeruhi 11 huku wawili kati yao wakiwa watoto, nane ni watu wazima na watano wamehamishiwa KCMC, kwa matibabu zaidi kutokana na hali yao.

# Kanisa lamwalika Samia jubilee miaka 50

**Na Halfan Chusi**

KANISA la Africa Inland Tanzania (AICT), Pastoreti ya Magomeni mkoani Dar es Salaam, limemwalika Rais Samia Suluhu Hassan katika jubilee ya miaka 50.

Sambamban na mwaliko huo, kanisa hilo limeahidi kutoa ushirikiano katika kuimarisha umoja, amani na utulivu nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari, katika viwanja vya kanisa hilo jana, Askofu wa AICT Dayosisi ya Pwani, Philipo Mafuja, alisema lengo la mwaliko huo ni kuendesha harambee ya kukamilisha ujenzi wa kanisa Sh. milioni 300.

"Tunatumia nafasi hii kuwaarifu mamilioni ya waumini wa kanisa la AICT kila mahali nchini kujumuika nasi iifikapo Oktoba 27, mwaka huu, hapa kanisani Magomeni.

"Ninaomba kutumia fursa hii pia kumkaribisha sana Mheshimiwa Rais Samia, ambaye ametupatia heshima kubwa kushiriki nasi siku hiyo pamoja na wengine wote watakaoambatana naye kuja kufanikisha harambee hii," alisema.

Askofu Mafuja aliwashukuru Watanzania wa dini na madhehebu tofauti waliopokea kadi za michango ya sadaka ya ujenzi wa kanisa hilo, sambamba na waliotoa ahadi ya kuchangia.

Alisema kuelekea siku hiyo, kutakuwapo na shughuli zingine za kijamii za kuonesha matendo ya huruma hasa kwa wale wenye uhitaji.

Pia alisema kanisa limepanga kugawa mitungi ya gesi kuunga mkono mpango wa serikali katika matumizi ya nishati safi ya kupikia na kutembelea vituo vya watoto yatima kuwajulia hali na kushirikiana nao.

Alisema miaka 50 ya kanisa imekuwa ya baraka kwa Watanzania kiroho na kimwili, kwa kuwa wameanzisha huduma katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwamo shule ambazo zimetoa mchango chanya katika maendeleo ya elimu.

Katika hatua nyingine, Askofu Mafuja aliwasihi wananchi kushiriki kujiandikisha na kupigakura katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwezi ujao, ili kuchagua viongozi wanaoona wanafaa kuwaongoza.

RIPOTI MAALUM

# Watoto walivyogeuka kitegauchumi mitaani

## -Hutumika kuchangisha fedha za makanisa na misikiti, wazazi, viongozi wa dini wang'aka

Na Waandishi Wetu

FIKIRIA mtoto mwenye umri wa kwenda shuleni, badala ya kuwa darasani au nyumbani akijisomea, yuko mtaani akipita mitaa kwa mtaa kuomba fedha za michango kwa ajili ya ujenzi wa makanisa, misikiti au ununuzi wa gari la mchungaji.

Ni maisha ya kila siku ya watoto wenye umri wa kuwa shuleni, kabla au baada ya masomo kukutwa katika mitaa mbalimbali wakiwa na karatasi mkononi lenye jina la taasisi fulani, wakisimamisha watu barabarani kuomba fedha za michango.

Hayo yanafanyika wakati Sheria ya Mtoto Sura Namba 13 Toleo la 2014, Kifungu (a) namba 12, kikizuia mtu yeyote kumwajiri au kumfanyisha mtoto kazi ambazo zinaweza kuwa na madhara kwa afya, elimu, akili, mwili au kwa maendeleo ya kimaadili ya mtoto.

Kifungu hicho kikisomwa pamoja na namba 14 kuhusu adhabu, kinaeleza kuwa mtu atakayekiuka kifungu chochote katika sehemu hiyo, atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atalipa faini isiyozidi Sh. milioni tano au kifungo cha miezi isiyozidi sita au vyote kwa pamoja.

Katika mahojiano maalum na waandishi wa habari hii yaliyofanyika maeneo tofauti katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, baadhi ya watoto wamekiri kufanyika kazi hiyo.


**WATOTO WANENA**

Mtoto X, mkazi wa jijini Mwanza na mwanafunzi wa darasa la sita katika shule ya Msingi Igelegele, anasimulia kwamba wanapatiwa fomu za michango kanisani ili kuchangisha fedha mitaani kwa ajili ya ujenzi wa kanisa na wakati mwingine kukiwa na shughuli zingine za kimaendeleo.

"Mara nyingi tunapewa fomu hizo wakati wa mafundisho na unapopewa huwezi kukataa kwani ni maelekezo ya mwalimu ambaye anasema ni mpango iliowekwa na uongozi wa kanisa ili kufikia malengo ya ujenzi husika. Mara nyingi tunazunguka wengine huchanga na wengine hukataa," anasema.

Mwanafunzi wa Kidato cha Kwanza (jina linahifadhiwa) katika Shule ya Sekondari ya Ngara, anakiri kupewa fomu ya kuchangisha kwa ajili ya kwenda kwenye maombi nje ya mkoa.

Anasema pamoja na kupewa fomu hiyo, mwalimu wao wa dini huwa anawaelekeza mahali pa kwenda kuchangisha michango hiyo ikiwa ni pamoja na kanisani, kwa ndugu zao wa karibu na rafiki.



Mwanafunzi mwingine wa kidato cha tatu shuleni hapo (jina linahifadhiwa), anasema alipewa fomu na mwalimu wa malezi wa dini ili kuchangisha mtaani fedha za kongamano la kitaifa.

Anasema jukumu hilo halimwathiri kielimu kwa kuwa anatumia muda wake ipasavyo kukusanya michango na kisha kuendelea na masomo.

**WAZAZI WAFUNGUKA**

Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, baadhi ya wazazi wamesema vitendo hivyo vinatweza utu wa watoto hao kutokana na kuzunguka maeneo mbalimbali wakiomba fedha bila kujali hali yao na hatari wawapo mitaani ambako magari, bajaji na pikipiki hupita.

Mkazi wa Ihayabuyaga Magu, mkoani Mwanza, Sara Tito, ambaye pia ni msusi, anakiri katika eneo lake la kazi kupokea watoto wa namna hiyo na kwa kwa wiki hupokea wastani wa watoto watatu.

Anasema mara nyingi wanapita na fomu za michango ya sherehe za kwaya, ujenzi wa makanisa na misikiti, huku wengine wakitumwa na wanaodaiwa kuwa wazazi, kutafuta fedha za matibabu kwa watoto wenzao.

"Saluni kwangu mara kwa mara wanapita, wengine wanahitaji michango ya mahafali, na ujenzi wa makanisa. Kama juzi alipitia mtoto akiomba mchango wa mtoto kuwa yuko hospitalini anahitaji matibabu. Kwangu mimi naona si sahihi kuwatumia watoto kwenye shughuli hizi," anasema.

Mkazi wa jijini Mwanza, Emmanuel Kido, anasema katika biashara yake ya duka, amekuwa akiwapokea watoto mara nyingi wakiomba kuchangiwa ujenzi wa misikiti, makanisa na vyumba vya madarasa na michango ya mahafali huku wakitaja baadhi ya viongozi wa maeneo husika kuwatuma wakiwa na ushahidi wa mihuri katika fomu zao.

Naye mkazi wa Mtaa wa Bariadi, Manispaa ya Kahama, Agatha Juma, anasema kuna watoto wengi mitaani wenye umri wa kwenda shuleni lakini wanatembea na fomu za kuomba michango ya ujenzi wa makanisa, ununuzi wa gari la mchungaji na mahafali, jambo ambalo ni kudhalilisha madhehebu na utu wa watoto husika.

Anasema huenda viongozi wa madhehebu hayo hawafahamu na badala yake kunaibuka kikundi cha watu wachache ndani ya makanisa na misikiti kinawatumia watoto kujipatia fedha, na kuwataka viongozi hao kuangalia namna ya kudhibiti suala hilo, lisiendelee kujitokeza katika jamii.

Mkazi wa Nyihogo, Zabroni Allex, anasema kuna wakati amekuwa huwakamata na kuwahoji wanapata wapi muda wa kwenda shuleni, kujisomea na wengi huzunguka mitaani kipindi cha mapumziko na wakati wametoka shuleni jioni.

Merania Marashi, mkazi wa Kata ya Mahina, Mwanza, anasema suala hilo linakera. Kila siku watoto wakitoka shuleni wakishakula huenda mitaani kuchangisha fedha, wengine wakidai kutumwa shuleni, makanisani na misikitini.

"Kila siku tunakemea ukatili majumbani. Lakini makanisani, misikitini huko nako kumekuwa chanzo cha ukatili. Unapomtuma mtoto mitaani akachangishe fedha unategemea nini?

"Kama si kutengeneza kizazi ambacho kitakuja kuwa hatari kwa taifa, maana uadilifu hautokuwapo kutokana na watoto kujua matumizi ya fedha wakiwa bado wadogo na wakati mwingine, kukutana na vishawishi huko mitaani," anasema Marashi.

**VIONGOZI WA DINI**

Baadhi ya viongozi wa dini pamoja na serikali waliotafutwa kuelezea suala hilo wanasema suala hilo sio la kiungwana na kuwakemea wanaofanya hivyo ya kuwa wanakiuka sheria ya mtoto.

Mchungaji wa Kanisa la Anglikana, wilayani Kahama, Esron Yuda, anasema ni kosa kuwatumia watoto katika kukusanya michango ya aina yoyote mitaani na kuahidi kulisemea jambo hili kanisani hasa siku za ibada, ili kama lipo walikemee lisiendelee kujitokeza, kwani linadharirisha imani zao.

Shekhe wa Wilaya ya Kahama, Alhaji Omary Damka anasema, wanapohitaji michango ya kuendeleza dini huwa wanatumia kamati maalum ambazo huandaliwa kwa ajili ya kukusanya michango na si kutumia watoto.

Anasema maendeleo yanohitaji kushirikisha jamii lakini si kwa kutumia watoto kupita mitaani kuchangisha fedha.

"Watoto wanahitaji uangalizi katika malezi, kuhimizwa kusoma kwa ajili ya maisha ya baadaye na husaidia kutojiingiza katika vitendo viovu," anasema.

Mwanasheria ambaye pia ni Kaimu Katibu Mkuu wa Shirika la Kutetea Haki za Binadamu (SHIHABI), Onesmo Daudi, anasema si sahihi kwa watoto kutumika kutafuta michango ya ujenzi wa makanisa na ununuzi wa magari ya wachungaji wao.

Anasema mzazi, mlezi au taasisi yoyote ya kidini hairuhusiwi kumbebesha majukumu mtoto kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Namba 21 ya Mwaka 2009 na endapo atabainika atachukuliwa hatua za kisheria, hivyo majukumu yanamnyima mtoto fursa ya kwenda shule kusoma.

Daudi anasema wanalaani vitendo vya namna hiyo kwa kuwa hali hiyo mara nyingi imekuwa ikijitokeza katika madhehebu yanayochipukia.

Anawasihi wenyeviti wa serikali za mitaa kuwachukulia hatua viongozi wa dini wanabainika kuwatumikisha watoto.

Ofisa Elimu Wilaya ya Ngara, James John, anasema ofisi yake haijapokea taarifa zozote za wanafunzi kushiriki katika kukusanya michango hiyo wakati wa masomo na kuwa, kama litakuwa linafanyika ni nje ya muda wa masomo wakati wa likizo au baada ya kutoka masomoni, wakiwa mikononi mwa wazazi.

John anakemea vitendo hivyo na kueleza kuwa mtoto anatakiwa kupata nafasi ya kupumzika na kutafakali aliyojifunza shuleni na siyo kushiriki katika kusambaza fomu za michango ya namna hiyo.

**• Imeandaliwa na Shaban Njia (KAHAMA), Rose Jacob (MWANZA), Neema Emmanuel (MWANZA), Vitus Audax (MWANZA), Judith Julius (NGARA)**

# Majaliwa ahamasisha wananchi kutumia fursa leo kujiandikisha

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amejiandikisha katika Daftari la Wakazi, kwa ajili ya uchaguzi viongozi wa Serikali za Mitaa katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu na kuhamasisha ambao bado kutumia fursa iliyobaki leo (Jumapili).

Majaliwa ambaye alifuatana na mke wake, Mama Mary Majaliwa, alijiandikisha jana katika kituo cha kujiandikisha kilichoko Shule ya Msingi Nandagala iliyoko Kitongoji cha Nanguruwe, Ruangwa mkoani Lindi.

Akitoa taarifa ya uandikishaji, Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo la Ruangwa, Frank Chonya, alisema wilaya hiyo ina tarafa tatu, kata 22, vijiji 90 na vitongoji 435 ambavyo vitahusika katika uchaguzi huo.

Chonya alisema wilaya hiyo imekadiria kuandikisha wakazi 123,803 na kati yao 60,188 ni wanaume na 63,615 wanawake.

Alisema hadi kufikia juzi, wameandikisha jumla ya watu 103,468 kati yao, wanaume ni 47,664 na wanawake ni 55,804.

"Mchakato wa uandikishaji unaendelea hadi kesho (leo) saa 12 jioni," alisema Chonya.

Akizungumza na wananchi waliokuwapo kituoni hapo, Majaliwa ambaye pia ni Mbunge wa Ruangwa, aliwashukuru viongozi wa Serikali za Vijiji wa Kata ya Nandagala kwa kuhamasisha watu kujitokeza kujiandikisha na kuifanya kata hiyo kuwa ya kwanza kwa uandikishaji katika jimbo hilo.

"Kazi ya uandikishaji inaendelea nchi nzima na mwisho wa uandikishaji ni kesho (leo). Tuwahimize wengine ambao bado hawajajiandikisha, nao pia waje kujiandikisha," alisema Majaliwa.



Mkuu wa Shule ya Sekondari Naisinyai, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Mbayani Kivuyo (katikati), akicheza kwaito na wahitimu wakati wa mahafali ya 16 ya kidato cha nne, shuleni hapo, jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wachimbaji madini wampa tuzo Rais Samia

**Na Thobias Mwanakatwe,** CHUNYA

WACHIMBAJI wa madini katika mikoa ya Songwe na Mbeya, kwa kushirikiana na kampuni ya MC Edwin Luvanda Branding and Entateiment, wamemtunuku tuzo Rais Samia Suluhu Hassan, kutambua mchango wake katika kukuza sekta ya madini nchini.

Tuzo hiyo waliikabidhi juzi kwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, wakati wa hafla ya usiku wa dhahabu iliyofanyika wilayani hapa na kuwashirikisha wachimbaji madini kutoka mikoa ya kimadini ambayo ni Mbeya, Chunya na Songwe.

Mkurugenzi wa kampuni hiyo iliyoandaa tuzo hiyo, Edwin Luvanda, alisema wameamua kutoa tuzo hiyo kwa rais, kwani amekuwa mstari wa mbele katika kukuza sekta ya madini, hivi sasa wachimbaji wananufaika madini ukilinganisha na huko nyuma.

Nao Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Mbeya, Njumbo Mtawa na Kaimu Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Songwe, Goodluck Mungure, walisema serikali imefanya kazi kubwa kuinua sekta ya madini ambapo hivi sasa kuna soko la uhakikika la kuuza madini hapa nchini.

"Zamani mfano sisi wachimbaji dhahabu tulikuwa tukilazimika kusafiri kwenda Dar es Salaam au mkoani, kwa ajili ya kwenda kuuza madini hali ambayo ilikuwa hatari kiusalama usumbufu huo hivi sasa haupo masoko yanapatikana karibu," alisema Mtawa.

Naye Homera alisema kwa kutambua kuwa dhahabu ni uchumi, biashara na pia ni maisha atawaelekeza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), wafike kutoa elimu kuhusu kodi mpya ya asilimia mbili wanayotozwa wachimbaji, ili wawe na uelewa mzuri.

"Alikuja Kamishna wa TRA mkoani kwetu, alifika hadi kwenye mpaka wa Kasumulu wilayani Kyela na kuahidi kushughulikia changamoto zote zinazowakabili wachimbaji," alisema.

Homera alipongeza kampuni ya MC Edwin Luvanda Branding and Entateiment, kwa kuandaa maonesho ya vifaa vinavyotumika kwenye uchimbaji pamoja hafla ya usiku wa dhahabu na kwamba yatafanyika mjini Mbeya.

Aidha, Homera aliwataka wachimbaji wa madini wakipata pesa zinazotokana uchimbaji wazitumie, kwani hakuna atakayeishi milele hapa duniani.

"Ukipata pesa kula maisha hakuna atakayeishi hapa duniani milele," alisema Homera na kuwatangazia wachimbaji hao kuwa mkoa umeandaa festiva 2024 ya nyama choma, itakayofanyika ufukwe wa Matema, Ziwa Nyasa wilayani Kyela," alisema.

# Hifadhi Serengeti, Mlima Kilimanjario zaibuka kidedea

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Balozi Pindi Chana, amezipongeza hifadhi za Serengeti na Mlima Kilimanjaro, kwa kushinda tuzo za utalii za Bara la Afrika, huku akimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kuendelea kuitangaza sekta ya utalii duniani kupitia Filamu ya Tanzania: The Royal Tour na Amazing Tanzania.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Hassan Abbasi, Taasisi ya Tuzo za Dunia za Utalii Kanda ya Afrika (World Travel Awards Africa - Gala), imeitangaza Tanzania kuwa nchi inayoongoza kwa kuwavutia watalii barani Afrika mwaka 2024 na Bodi ya Utalii Tanzania kuwa bodi inayoongoza Barani Afrika mwaka 2024.

Aidha, taasisi hiyo imezitangaza hifadhi mbili za Serengeti na Mlima Kilimanjaro, kuwa washindi kwenye kipengele cha Hifadhi na Kivutio Bora cha Utalii Barani Afrika mwaka 2024.

Hifadhi ya Taifa Serengeti imetangazwa kuwa mshindi katika kipengele cha Hifadhi Bora Barani Afrika (Africa's Leading National Park 2024), wakati Mlima Kilimanjaro ikitangazwa Kivutio Bora cha Utalii Barani Afrika (African Leading Tourism Attraction 2024)

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Serengeti imezishinda hifadhi zingine kwa ubora barani Afrika, ilizoshindanishwa nazo ambazo ni Maasai Mara ya Kenya, Kruger ya Afrika Kusini, Central Kalahari ya Botswana, Etosha ya Namibia na Kidepo Valley ya Uganda.

Mlima Kilimanjaro umevishinda vivutio vingine vya utalii ambavyo ni Hifadhi ya Ngorongoro, Hartbeespoort Aerial Cableway, V&A, Waterfront, Robben Island, Table Mountain zote za Afrika Kusini. Pia Ziwa Malawi, Okavango Delta ya Botswana na Pyramid of Giza ya Misri.

Taarifa hiyo pia ilisema Mlima Kilimanjaro umeshinda tuzo hiiyo ya kivutio Bora Barani Afrika mara sita, kuanzia mwaka 2013, 2015, 2016,2017, 2018 na sasa 2024 huku Hifadhi ya Serengeti nayo imeshinda mara sita mfululizo kuanzia mwaka 2019.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wananchi watumie siku ya mwisho kujiandikisha kwa uchaguzi wa mitaa

**KAZI** ya kujiandikisha kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa inafikia tamati leo. Wakati mchakato huo ukiwa katika lala salama, viongozi wakuu kitaifa wamekuwa wakiwahimiza wananchi kushiriki mchakato huo, ili kuwa na sifa za kuwachagua viongozi wanaofaa.

Viongozi hao si tu wanafanya hivyo kinadharia bali kwa vitendo, kwa sababu wameshuhudiwa wakijiandikisha katika maeneo yao, ili nao washiriki kuwachagua watu watakaosimamia shughuli za maendeleo na kuwaongoza wananchi kutatua changamoto zilizoko kwenye sehemu husika.

Katika kufanya hivyo, wakati wa kufunguliwa kwa pazia la kujiandikisha, Rais Samia Suluhu Hassan, alifanya hivyo Chamwino mkoani Dodoma huku Makamu wa Rais, Dk Philip Mpango, akijiandikisha nyumbani kwao, Buhigwe mkoani Kigoma. Mbali na Rais na makamu wake, viongozi wengine kama vile mawaziri na wakuu wa mikoa wamejiandiskisha huku wakiwataka wananchi waige mfano huo.

Aidha, jana Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alijiandikisha Ruangwa mkoani Lindi, ikiwa imabaki siku moja na kuhimiza wananchi kutumia siku ya leo kujiandishisha kwa ajili ya uchaguzi huo.

Licha ya kujiandikisha, viongozi hao wameeleza umuhimu wa kujiandikisha na kushiriki uchaguzi huo na kuonya kuwa asiwapo mtu yeyote wa kufanya hujuma katika mchakato mzima. Rais Samia, kwa mfano, ameonya mara kadhaa kuhusu dosari zozote zitakazojitokeza, huku akitaka uchaguzi huo usilitie taifa doa.

Matamko hayo ya viongozi yameonesha kwamba Hakuna jambo lolote la ajizi katika mchakato mzima, bali kinachotakiwa ni sheria kufuatwa, ili uwe huru na haki na pia haki itendeke ndani ya vyama katika uteuzi wa wagombea na usimamizi unaozingatia demokrasia na utawala bora.

Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopangwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu, ni wa muhimu sana kwa wananchi. Kwa mantiki hiyo, wale ambao hawajajiandikisha wanapaswa kufanya hivyo, ili kutumia haki yao ya kuchagua viongozi wanaofaa ambao watawaongoza kwa miaka mitano ijayo.

Kama Rais Samia alivyosema wakati wa kilele cha Mwenge wa Uhuru na Kumbukumbu ya Miaka 25 ya Kifo cha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, jijini Mwanza, uchaguzi wa serikali za mitaa ni wa muhimu, kwa sababu ni chimbuko la demokrasia na utawala bora. Pia ni jukwaa la wananchi katika kupata viongozi bora watakaoshirikiana nao katika kubuni, kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo na kutatua kero zinazowakabili katika maeneo yao.

Kwa hiyo, uchaguzi huu ni wa muhimu zaidi na viongozi watakaopatikana katika mchakato huu, ni wale wanaofahamika na wananchi na ni watu wa karibu katika kutatua matatizo yanayoikabili jamii kwa haraka kuliko wanaotoka ngazi za juu kama vile wilaya, mikoa na taifa.

Wakati leo ni siku ya mwisho, ni vyema wananchi wakajitokeza kujiandikisha na wala wasipuuze wito unaotolewa na viongozi wa kitaifa mara kwa mara wanapokuwa kwenye ziara au shughuli zao za kila siku.

Kama wasemavyo wahenga majuto ni mjukuu, ni vyema wananchi wakashiriki kujiandikisha na hatimaye kupiga kura kuwachagua viongozi wa, badala ya kuendelea kwa chukulia jambo hilo kwa mazoea. Mara nyingi baadhi ya wananchi katika maeneo mbalimbali wamekuwa hawashiriki kupiga kura na matokeo yake, wanapopatikana viongozi wasiofaa, huwa wa kwanza kutoa lawama.

Kila mwananchi ambaye ana uchungu na matatizo katika eneo lake, ni vyema akashiriki mchakato huu, kwanza kwa kujiandikisha leo ambayo ni siku ya mwisho, kushiriki kampeni za vyama vya siasa, ili kusikiliza sera zao na hatimaye kupiga kura siku itakapowadia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mkakati wa kudhibiti rushwa ubebwe na somo la maadili

Na Sabato Kasika

**RUSHWA** ni adui wa haki. Ni adui wa utu na heshima ya mtu, kwani imekuwa ikisababisha baadhi ya watu kukosa haki na hivyo kuzuia vilio katika maeneo mbalimbali na hata sehemu za kazi.

Kushamiri kwa rushwa katika maeneo mbalimbali, kunanishawishi kusema kuwa kuna haja ya kuwapo kwa somo la maadili shuleni, ili kuwaandaa watoto kupiga vita ya rushwa ya ngono wangali wadogo.

Ikumbukwe kuwa, kila mwaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), anapofanya ukaguzi na kutoa taarifa kwa umma, 'upigaji' mwingi wa fedha za umma umekuwa ukidhihirika wazi.

Upigaji huo hufanyika katika taasisi za umma, huku chanzo chake kikiwa ni ambayo kwa namna moja au nyingine, inachangia kukwamisha shughuli za maendeleo kwa mtu mmoja, jamii na taifa kwa ujumla.

Kushamiri kwa rushwa, kuna chimbuko lake ambalo ni mmomonyoko wa maadili unaoanzia katika ngazi ya familia hadi taifa. Hivyo, ingekuwa vyema kama kungekuwa na somo la maadili shuleni.

Mmomonyoko ndio unaozaa maovu na kuenea kwa rushwa ambayo sasa ni sugu katika maeneo mbalimbali na kusababisha jamii kukosa haki, huku baadhi ya watoaji na wapokeaji wakineemeka.

Wakati jitihada za kupambana na rushwa zikiendelea, ninaona ni muhimu kuwa na mitaala, kwa ajili ya somo la maadili, ambalo linaweza kusaidia wanafunzi kuitambua rushwa wangali wadogo.

Kupitia somo hilo, wanafunzi wanaweza kujua rushwa ni nini, ikiwamo ya ngono, fedha na vitu vingine badala ya kuisikia tu bila kujua maana yake na madhara yake na kujikuta wakijiingiza humo.

Wanafunzi wakipata elimu kuhusu rushwa na madhara yake, watakapokuwa watu wazima wataendelea kuichukia, kwani ndio inayokwamisha maendeleo yao na nchi kwa ujumla.

> **Wanafunzi wakipata elimu kuhusu rushwa na madhara yake, watakapokuwa watu wazima wataendelea kuichukia, kwani ndio inayokwamisha maendeleo yao na nchi kwa ujumla.**

Si vibaya ukawekwa mkakati wa kuanzisha somo hilo kwa shule za msingi hadi juu, ili wanafunzi wapate elimu kuhusu rushwa, kwani ni miongoni mwa mambo ambayo yanachangia mmomonyoko wa maadili.

Ninaunga mkono juhudi mbalimbali ambazo zimekuwa zikifanywa za kupambana na rushwa, ikiwamo kuanzisha klabu za wapinga rushwa shuleni, ili wanafunzi wapate elimu ya madhara ya tatizo hilo.

Hatua hiyo ni nzuri kwa sababu inaweza kuwandaa wanafunzi kupinga rushwa wangali wadogo hata pale wanapokuwa watu wazima wataendelea kupambana nayo kwa manufaa yao na ya taifa kwa ujumla.

Lakini wakati vita hii ikiendelea, suala la kuwa na somo la maadili ninadhani ni la muhimu, kwani linaweza kusaidia wanafunzi kutambua mambo mbalimbali yanayohusiana na maadili mema.

Kama nilivyoeleza awali kuwa taarifa za kila mwaka za CAG, zimekuwa zikionesha upigaji mwingi wa fedha za umma, hivyo ni muhimu kuwapo mikakati mbalimbali ya kuwaandaa vyema wanafunzi, ikiwamo somo la maadili.

Kwa kawaida, viongozi na watumishi bora wa umma, huandaliwa tangu mwanzo, hivyo kuanzisha somo la maadili shuleni linaweza kusaidia kuandaa viongozi watakaoleta mapinduzi chanya ya maendeleo ya nchi.

Utaratibu wa utoaji wa elimu kuhusu madhara ya rushwa kutolewa kuanzishwa shule za msingi, ni mtazamo unaolenga kuhakikisha rushwa inaondolewa nchini kuanzia sasa na hata baadaye.

**MAKALA**

**FIKRA MBADALA**

# Hongera Spika Tulia, umeonesha unaweza



**Pascal Mayalla**

HIZI ni pongezi za dhati kwa Spika wa Bunge la Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge dDuniani (UPU), Dk. Tulia Ackson. Pongezi hizi zinatokana na alivyowajibu kwa kuwakemea waandishi wa nchi mabeberu, walioanza kumsakama kukutana na Rais wa Russia, Vladmir Putin.

Spika Tulia, ameonesha uwezo huo akiwa nje ya nchi. Swali ni kama ameweza kuonesha uwezo huo akiwa nje ya nchi, nini kinamfanya asioneshe kwenye kuisimimia serikali yetu kupitia Bunge lake?

Hapa ninauzungumzia huo uwezo mkubwa wa Dk. Tulia aliouonesha hivi karibuni kati, akiwa nje ya nchi na kujiuliza ni kwa nini auoneshe uwezo wake huo kule badala ya hapa nyumbani wakati ni jukumu la mhimili wake kuisimamia serikali yetu? Je, tumshinikize kuonesha uwezo huo hapa nyumbani tena kwa kuanza na Bunge letu kuitekeleza ile hukumu ya Mahakama ya Rufani, kuhusu ubatili wa Katiba yetu na sheria zetu?

Spika Tulia ni mwanasheria. Kwa nini Bunge letu liendelee kututungia sheria batili zinazokwenda kinyume cha katiba? Kitendo cha kumpa Rais wetu kutia saini sheria batili kinyume cha Katiba, kitakuja kutokea kwa wabunge makini ambao watahitaji Ibara ya 46A ya Katiba yetu itekelezwe. Kwa nini huu mhimili wetu wa Bunge utufanyie hivi wakati uko chini ya mwanasheria nguli, mbobezi na mbobevu?

Japo Rais Samia Suluhu Hassan anaitwa zaidi mama, kwa umri wangu mimi ni Dada (mimi ni mtu wa umri wa miaka 60) na Dk. Tulia ni mdogo kwangu, hivyo mimi nawaita madada wawili, mtu na dada mtu au mtu na dada yake. Mmoja ni dada mkubwa, mwingine ni dada mdogo.

Mhimili mkuu kabisa ni dola unaoongozwa na Dada Mkubwa Rais Samia. Mhimili wa pili kwa ukubwa ni Bunge unaoongozwa na Dada mdogo, tena almanusra na ule mhimili wa tatu, kama tusingepindisha kidogo katiba, Jaji Mkuu aendelee kuwa CJ licha ya kutimiza umri wa kisheria wa kustaafu kwa mujibu wa Katiba.

Kwenye mhimili ule pia ilikuwa aingie mwanamke, hivyo tungekuwa chini ya madada watatu, yaani 'Three Sisters'. Ili kuliepuka hili, imebidi katiba ipindishwe kidogo, Jaji Mkuu aendelee kidogo, ili kuipusha mihimili yote mitatu kuwa chini ya madada watatu.

Naomba kuanza na maslahi yangu, Dada Mdogo ni mwalimu wangu wa sheria, mwaka wa kwanza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), somo letu la kwanza, hivyo naomba usijekuonekana hapa ni mwanafunzi anampigia promo mwalimu wake, ili ndiye awe yeye kwenye lile jambo letu.

Mwaka 2019, niliandika makala ya 'Voices from within: Nimesikia sauti, Dr. Tulia Ackson ndiye Spika ajaye! Sauti hiyo imenieleza Ndugai, japo atatamani aendelee lakini nilikuwa naandika kitu fulani. Mara ghafla nikasikia sauti ndani mwangu ikiniambia kuwa "Spika ajaye ni Dk. Tulia Ackson.

Sauti hiyo ikaniambia japo Ndugai, atakuwa anatamani sana kuendelea kuwa Spika, hatakuwa kwa sababu fulani (japo sauti hiyo imenieleza hizo sababu za kwa nini Ndugai hataendelea kuwa Spika Bunge lijalo.

Lakini si lazima kusema kila unachosikia, kwa sababu wakati mwingine si kila unachosikia ndani mwako ni sauti kutoka kwa Mungu au ni maono. Sauti nyingine ni sauti za shetani tu na si sauti za Mungu kama zilivyo ndoto zingine. Ni ndoto za shetani.

Ukisikia sauti ukahisi inaweza isiwe sauti ya Mungu au ukiota ndoto ya jambo la ajabu ajabu ukahisi jambo hilo si la kheri, si lazima uliseme.

Baada ya Spika Samuel Sitta, hali imeonesha kwamba kiti cha Spika ni cha muhula mmoja, hiyo ikiisha, Naibu Spika ndiye huwa Spika. Wakati wa Spika Sitta, Naibu Spika alikuwa Anna Makinda. Japo Sitta alitamani kuendelea, aliwekwa pembeni. Naibu wake Makinda akachaguliwa kuwa Spika.

Wakati wa Spika Makinda, Ndugai alikuwa Naibu Spika na baada ya kumaliza kipindi kimoja, Ndugai akawa Spika, hivyo hali zinaelekeza baada ya Spika Ndugai, moja kwa moja Spika anayefuatia ni Naibu Spika Dk. Tulia.

Hivyo, ilipojitokeza fursa ya uspika, nilisema Kujiuzulu kwa Ndugai ni mpango wa Mungu kwa Tanzania, ili tupate Spika Bora. CCM itateua Spika Bora au Bora Spika kama kawa? Dk. Tulia alipoukwaa uspika hatukumkopesha. Nilisema Je, wajua, Naibu Spika, chini ya "Bora Spika" anaweza Kuwa "Spika Bora?" Dk. Tulia, Ukitulia, Una Fursa ya Kuwa Spika Bora Sana", Hongera Sana.

Na kweli Spika Tulia alipoingia akaanza moto wake nikasema Spika Dk. Tulia yuko sahihi sana, CHADEMA wajifunze kufanya vitu kwa usahihi na wafanye kiusahihi

Pamoja na mazuri yake yote, Dk. Tulia pia ni binadamu. Anaweza kukosea, hivyo alipokosea kwenye madudu ya IGA ya DPW na bandari zetu, tulimpa "IGA ya DPW imetusaidia sana kujitambua. Tuna wanasheria wa aina gani! Bunge na Serikali yetu ilipitishaje IGA hii?

Mazuri yake, yameendelea na tumeendelea kumpongeza na kushauri. Hongera Spika Dk. Tulia. Kuna haja maspika wetu iwe lazima kuwa wanasheria? Na alipoukwaa urais wa IPU ndiyo funga kazi. Juzi kati kafunga kazi kwa kuwawakia mabeberu kutudharau Afrika kuwa hatuwezi.

**Mungu ibariki Tanzania**
**Paskali**
**+255 754 270403**

# Ujenzi bomba la mafuta wafikia asilimia 45

**Na Shaban Njia, NZEGA.**

UTEKELEZAJI wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani, mkoani Tanga, Tanzania umefikia asilimia 45 huku ujenzi wa kiwanda cha kuweka mifumo ya kutunza joto kwenye mabomba yanayotumika kusafirisha mafuta hayo, ukikamilika kwa asilimia 93.

Naibu Katibu Mtendaji wa Tume ya Kitaifa ya Mipango inayosimamia masuala ya Menejimenti ya Mradi ya Maendeleo, Dk. Linda Ezekiel, alisema hayo jana wakati wa ziara ya kukagua kiwanda hicho kilichoko katika kijiji cha Igusule, Nzega mkoani Tabora.

Alisema Kamati ya ufundi inayosimamia madeni na Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), wameridhishwa na kazi inayoendelea na kuwa wanatarajia ukamilike ifikapo mwaka 2026 kama mkataba unavyoelekeza. Dk. Ezekiel alisema mabomba 86,000 yatawekewa koti ya joto, ili kurahisisha usafirishaji wa mafuta ghafi na wamefurahishwa kuona asilimia 94 ya wafanyakazi ni wazawa na kuwataka kuwa waminifu kwa kuwa, serikali imewekeza fedha nyingi kwenye utekelezaji wake.

Mjumbe wa Bodi ya TPDC, Balozi Mstaafu Peter Kallaghe, alisema serikali za Tanzania na Uganda, zimetoa fedha nyingi kwenye utekelezaji wa mradi huo, hivyo ni vyema ukatekelezwa kwenye viwango walivyokubaliana kwenye mkataba, ili unufaishe nchi hizo.

Mratibu wa Kitaifa wa Mradi wa Bomba la Mafuta kutoka TPDC, Asiad Mrutu, alisema utekelezaji wa mradi unaendelea vyema na hakuna ukosefu wa fedha katika utekelezaji wake na mpaka sasa zimetumika Sh. bilioni 977.

"Mabomba yznye urefu wa kilometa 1,004 yameshafika kutoka China kati ya mabomba 1,443 yanayotakiwa kutumika kwenye mradi huu, hivyo mradi uko ndani ya muda wa utekelezaji wake na ifikapo mwaka 2026 utakuwa umekamilika," alisema Mrutu.

Alisema wananchi 9,858 kati ya 9,927 ambao walipitiwa na mradi wameshafidiwa maeneo yao, ili kupisha utekelezaji kati ya hao, 294 walijengewa makazi ya kudumu huku 69 wakiwa bado hajawalipwa kwa sababu ya masuala ya kifamilia ya mirathi na fedha zao ziko watakapokamilisha watalipwa.

Mrutu alisema kwa sasa wanaendelea na kazi ya kuweka mifumo ya kuhifadhi joto katika mabomba na kuyasafirisha maeneo mbalimbali ya utekelezaji wa mradi na zaidi ya vijana 500 wazawa wamepewa ajira zenye kuhitaji ujuzi na zile zisizohitaji, wananufaika na uwapo wa mradi huo.

# Masauni aagiza Jeshi la Polisi kutunza magari wanayokabidhiwa

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni, ameliagiza Jeshi la Polisi kutunza magari ambayo wamekabidhiwa.

Amesema magari yanayoendeshwa na madereva askari wa jeshi hilo kulinganisha na ya raia, yao huharibika haraka kana kwamba yote hukimbiza mwizi.

Amesema hatarajii mwananchi kupata shida na kwenda kituo cha polisi akaambiwa gari bovu au hawana usafiri wa kumfuatilia mhalifu ama kuambiwa aweke mafuta, wakati serikali imeyateremsha hadi ngazi ya wilaya.

Waziri Masauni aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati wizara hiyo ikipokea magari 77 aina ya GWM P Series Double Cabin, ikiwa ni mwendelezo wa utekelezaji wa mkataba baina yake na Kampuni ya Ashok Leyland ya nchini India.

Magari hayo ni sehemu ya yalishapokewa mwaka jana idadi yake ikiwa ni 40 ya aina hiyo, huku mengine yanatarajiwa kuwasili hapo baadaye ili kukamilisha idadi yanayotakiwa kutolewa na kampuni hiyo.

Makabidhiano hayo yamefanywa na Kampuni ya Kifaru Motor Ltd, ambaye ni mwakilishi wa watengenezaji wa magari hayo na ni wawakilishi wa Kampuni ya Ashok Leyland, Mkurugenzi wake ni, Brigedia Generali Mstaafu Michael Luwongo (Rtd).

Akizungumza katika makabidhiano hayo, Waziri Masauni alisema; "Magari haya yatatumika vyema kusaidia kutoa huduma bora kwa wananchi."

Alisema lengo la msingi ni kuhakikisha wananchi wanahudumiwa vizuri na kulitaka Jeshi la Polisi kuhakikisha, fedha za walipakodi wanazithamini na kuzitunza.

"Itakuwa jambo moja la kusikitisha kwa leo mtu anapewa gari mpya kabisa alafu baada ya siku ya tatu tunalikuta limetundikwa juu. Hiyo ni kukosa huruma ya fedha za Watanzania maskini wa nchi hii wanaokatwa kodi, ili kulipa askari wetu wafanye kazi nzuri.

"Ikifika wakati wa matengenezo na bahati nzuri, Mkurugenzi wa Kampuni ya Kifaru amezungumza hapa kwamba, wako tayari kufanya matengenezo hayo," alisema.

Akitoa neno la shukrani, Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini, Inspekta Jenerali (IGP), Camillus Wambura, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa yote anayoendelea kufanya ndani ya Jeshi la Polisi, ikiwamo maboresho makubwa yanayoleta mapinduzi kwao.

"Mheshimiwa mgeni rasmi, tunaishukuru Wizara yako ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kusimamia sera na maendeleo ya wizara hii. kuhakikisha Jeshi la Polisi linakuwa la kisasa na kuheshimika ndani na nje ya mipaka," alisema.

IGP Wambura alitoa rai kwa viongozi waandamizi, maofisa na madereva ndani ya jeshi hilo, watakaokabidhiwa magari hayo, kuhakikisha wanazingatia kanuni za utumishi wa umma za utunzaji na usimamizi wa rasilimali hizo.

Aliwataka kuzingatia sheria za usalama barabarani, ili magari hayo yadumu kwa muda mrefu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Vita Kawawa, alisema magari hayo ni nyenzo muhimu kwa jeshi hilo, ili kupata tija iliyokusudiwa na kutaka yatumike kwa shughuli zilizokusudiwa.

Kawawa alisema magari hayo ni mapya na ya kisasa na hivyo kuagiza madereva wapate mafunzo ya kutosha, ili kuyatumia kama yalivyo.

Brigedia Jenerali mstaafu Luwongo, alisema Kampuni ya Kifaru inaahidi si kwamba imeleta magari hayo kisha kuyatelekeza, bali watakuwa karibu na watumiaji ambao ni Jeshi la Polisi, ili kuhakikisha yanakuwa katika ubora stahiki na hata kutoa ushauri wa kitaalam ikihitajika kufanya hivyo.

# Miaka 30 ESRF katika kuimarisha maendeleo ya kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Utafiti wa Masuala ya Kiuchumi na Kijamii (ESRF), imekuwa nguzo muhimu kwa maendeleo ya Tanzania, ikiiweka pamoja wataalamu, watunga sera na wananchi kuhakikisha zinatengenezwa sera za kiuchumi na kijamii zinazotekelezeka na zinazozingatia hali halisi.

Kwa miongo mitatu, ikiwa imeanzishwa mwaka 1994, ESRF imekuwa ikitoa utafiti wenye ushahidi wa kutosha, ili kuwajulisha waandaaji wa sera ngazi za kitaifa, kinachofaa kwa kuzingatia mazingira na aina ya mahitaji halisi.

"Tangu kuanzishwa, ESRF imekuwa ikitumia nguvu zake katika kukuza ufahamu wa umma kuhusu masuala ya kiuchumi na kijamii, kukuza mazungumzo kati ya waundaji sera, watafiti na mashirika ya jamii ya kiraia na kuongeza uwezo wa taasisi za Tanzania kufanya uchambuzi wa sera na usimamizi wa maendeleo kwa ufanisi," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa ESRF, Prof. Fortunata Makene, katika mahojiano yaliyofanyika hivi karibuni.

Akizungumza kabla ya maadhimisho ya miaka 30 ya taasisi hiyo yanayofanyika kesho (Oktoba 21), Prof. Makene alisisitiza michango muhimu ambayo ESRF imefanya, ikiweka kiwango cha juu kwa wengine kufuata.

"Taasisi yetu imefikia hatua muhimu katika maeneo haya, ikichangia njia ya maendeleo iliyojumuisha na yenye usawa kwa nchi," alisema.

Moja ya michango muhimu zaidi ya ESRF imekuwa ushiriki wake katika uundaji na ukaguzi wa sera na programu za kisekta katika nyanja mbalimbali zikiwamo fedha, nishati, kilimo, utalii na rasilimali za asili.

Utafiti wa taasisi hiyo, umetoa ufahamu muhimu kuhusu changamoto na fursa zinazokabili sekta hizo, kuwawezesha watunga sera kufanya uamuzi sahihi na kutekeleza hatua pangwa kwa ufanisi.

Pamoja na utafiti unaolenga sera, ESRF pia imekuwa ikishiriki kikamilifu katika mipango ya maendeleo na kuwapatia uwezo watu mbalimbali kwa lengo la kuendesha utafiti na kutekeleza.

Taasisi hiyo imetengeneza na kutekeleza programu nyingi za mafunzo. Miongoni mwa programu hizo ni vyeti vya uzamili, ushiriki wa kimataifa, na programu za mafunzo ya washiriki, ili kuwawezesha watu kuwa na ujuzi na maarifa muhimu kuchangia maendeleo ya Tanzania.

Kuna athari chanya kubwa na nyingi zilizosababishwa na utafiti mbalimbali unaofanywa na ESRF juu ya sera zinazotengenezwa. Matokeo ya utafiti wa taasisi hiyo, yamewajulisha watengeneza sera wa serikali kuhusu masuala mbalimbali, zikiwamo athari za mapato za leseni za biashara, ushirikiano kati ya serikali na wadadisi na mikakati ya kupunguza umaskini.



Mkurugenzi Mtendaji wa ESRF, Prof. Fortunata Makene

Taasisi hiyo, Prof. Makene anasema imekuwa na jukumu muhimu katika kukuza mazungumzo kati ya serikali na mashirika ya jamii ya kiraia, likikuza mchakato wa uundaji sera unaojumuisha zaidi na unaoshirikisha.

Prof. Makene alibainisha kuwa ESRF imehimiza ushirikiano kati ya wataalam wa Tanzania, kuwawezesha kuchukua hatua katika kukabiliana na changamoto za kiuchumi.

Alisema ESRF kwa miongo mitatu pia imesimamia mazungumzo ya sera na vyuo vikuu tofauti. Kwa mfano, mwaka huu, imeshirikiana na Chuo cha Maendeleo ya Kimataifa na Kilimo (CIDGA) katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha China, kuzungumzia uzoefu wa maendeleo ya kilimo cha mpunga kati ya Tanzania na China.

"Mada zilizojadiliwa wakati wa mkutano huo zilikuwa Mchakato wa Ugani wa Teknolojia ya Kilimo, Ushirikiano wa Maendeleo: Uzoefu wa Maeneo, Mfumo wa Kupunguza Umaskini na Jukumu la Taasisi za Utafiti wa Kisayansi na Wataalam katika kuimarisha mafanikio katika kilimo cha mpunga.

"Ukiangalia tafakari iliyotolewa na Prof. Li Xiaoyun kutoka CIDGA inabainisha zilikuwa muhimu sana katika kusaidia watengenezaji wa sera kutambua umuhimu wa kuweka viwango stahiki vya kisera kuinua kilimo," alisema Prof. Makene.

Mfano mwingine anasema Septemba, mwaka huu, ESRF chini ya makubaliano ya 'Impact Evaluation Lab' kwa msaada wa Hewlett Foundation, ilifanya mafunzo juu ya mbinu za tathmini ya athari kwa washiriki kutoka serikali, sekta binafsi, wanazuoni, taasisi za utafiti na mashirika yasiyo ya kiserikali.

Kwa kuwawezesha washiriki kutoka sekta mbalimbali kuwa na ujuzi wa kufanya tathmini za athari, ESRF imechangia njia ya uundaji sera inayotegemea ushahidi zaidi, husaidia waundaji sera kutambua hatua za ufanisi na kutenga rasilimali kwa ufanisi zaidi.

Mafunzo ambayo yaliunganisha washiriki kutoka sekta mbalimbali, yalikuza ushirikiano na ugawanyaji wa maarifa, washiriki hawa wanaweza kutambua na kushughulikia changamoto na fursa za kawaida wakati wa kupata ujuzi na maarifa muhimu ya kufanya tathmini za athari.

Kwa ujumla, mafunzo ya ESRF juu ya Mbinu za Tathmini ya Athari ni mpango muhimu ambao unaweza kuboresha sana ubora wa utafiti na uundaji sera nchini Tanzania.

Aidha, kwa kuwawezesha washiriki kwa ujuzi na maarifa muhimu, ESRF inachangia ajenda ya maendeleo inayotegemea ushahidi zaidi na yenye ufanisi.

"Kwa kuwawezesha washiriki kwa ujuzi na maarifa muhimu, ESRF inachangia ajenda ya maendeleo inayotegemea ushahidi zaidi na yenye ufanisi," alisema Prof. Makene.

Mfano mwingine wa mafanikio ni kutiwa saini kwa makubaliano (MoU) kati ya TanzaniaInvest, jukwaa kuu la mtandaoni la biashara kwa wanaopenda kuwekeza Tanzania na ESRF ili kuboresha ufuatiliaji na uwapo wa habari za kiuchumi zinazohusiana na uwekezaji nchini katika mikoa mbalimbali iliyoandaliwa miongozo.

"Kupitia ushirikiano huu, tunampa TanzaniaInvest taarifa zote za utafiti za kina za uchumi, data, na ufahamu. TanzaniaInvest itapata faida kutoka kwa jukwaa lake imara la mtandaoni na utaalamu, ili kuipeperusha maeneo mbalimbali, watu wa ughaibuni hapa nchini waweze kuvutia wawekezaji,

"Miongozo hii ya uwekezaji inakusudia kutoa ufahamu wa kina kuhusu fursa za kiuchumi za kikanda, mazingira ya uwekezaji na uchambuzi wa sekta maalum kote Tanzania, ili kusaidia wawekezaji, kwa hivyo kuwa na jukwaa la kuonyesha kutakuwa na faida kubwa kwa watu," alisema.

Prof. Makene alisisitiza namna ambavyo ESRF imejitolea kuhakikisha kwamba wanaweka msingi wa utafiti, ukweli katika ubora wa hali ya juu wa utafiti ambao hausababishi hasara wala kujivuta kama taifa.

"Kwa miaka 30, ESRF imebaki mstari wa mbele wa ajenda ya maendeleo ya Tanzania, ikitoa utafiti mbalimbali ulioshiba, ili kuongoza watengeneza sera.

Tunapotashauri hatua hii muhimu, tunatazama pia mbele, tukiwa na nia ya kushughulikia changamoto zinazoibuka za mazingira ya uchumi yanayobadilika kwa kasi," alibainisha Prof. Makene.

Alisema kwa kuangalia mambo ya baadaye, ESRF inatarajia kupanua ajenda yake ya utafiti, ili kujumuisha mwenendo mpya wa kiuchumi unaoibuka duniani na kuimarisha ushirikiano wake na jumuiya za mitaa na watunga sera, ili taifa lisikwame pasipotakiwa.

Taasisi hiyo itaendelea kuwa na jukumu muhimu katika kuhakikisha kuwa utafiti wake unawajulisha moja kwa moja waundaji sera katika ngazi zote za serikali.

ESRF inapoingia muongo wake wa nne, inatarajiwa kukabiliana na changamoto zinazoibuka kama vile mabadiliko ya hali ya hewa, kidijitali na usawa wa kijamii. Kujitolea kwa umakini kwa taasisi hiyo kwenye utafiti wenye ushahidi kunahakikisha kuendelea kukomaa kwa michango yake katika kuwezesha mustabali bora wa Tanzania.



Mkurugenzi Mtendaji wa ESRF, Prof. Fortunata Makene, akizungumza katika moja ya vikao vya ushirikiano wa kiuanazuoni na China, hivi karibuni jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

MAISHA
OKTOBA 20, 2024
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 13

**Yupia jeans ya kuchanika**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Fanya ubunifu bora wakati wa ujenzi wa nyumba



Ukurasa 12

**HARUSI**





# Unawezaje kuwa na ngozi laini?


Ukurasa 14

## WATOTO


### MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA









### FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
CHA, IBA, TANGA, ASALI, ACHIKA, LIMBUA


### TOA TOFAUTI 5




### AMSHA AKILI




## PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Juma alikuwa akicheza na wenzake upenuni mwa nyumba yao, mara alikatiza paka akiwa amemkamata panya mdomoni mwake.

Juma alionekana kushangaa tukio hilo na kumuuliza mwenzake.

**Juma:** Itakuwaje panya kakamatwa kirahisi kama vile?

**Tom:** Paka ana nguvu na akili nyingi anamkamata panya kwa haraka.

**Juma:** Basi atakuwa sio mjanja kama yule panya Jerry katika televisheni.

**Tom:** Ile ni katuni tu, lakini panya sio mjanja kuliko paka

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Akikwambia nimemwacha mke nitakuoa, jitafakari

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee kuelimishana kuhusu Maisha Ndivyo Yalivyo. Bado narudishwa kwenye anga la ndoa ambalo lina sekeseke nyingi. Leo darubini inawalenga wale walaghai katika ndoa.***

Wako watu wengi wenye uwezo kifedha, hupita huko na kule ndani ya nchi na hata nje ya nchi wakiwadanganya wanawake kuwa walishawaacha wake zao kitambo, hivyo wanatafuta mahusiano mapya.

Kumbe wanatafuta wanawake wa kujirusha wanapokuwa mbali na familia zao kibiashara na kadhalika, mtu anapokwambia nilishamwacha mke wangu kitambo na kugawana mali usimwamini hata kidogo, jitafakari kuepusha majuto.

Mwingine atamwapia mwanamke kwamba mke wangu alifariki dunia muda mrefu, hivyo natafuta mwenza mwingine kumbe ni uongo. Kuna kitu anataka kutoka kwa mwanamke huyo na akishakipata anatokomea kusikojulikana.

Yuko dada mmoja alikuwa ameolewa ndoa nzuri sana na kubahatika kuzaa watoto wawili, lakini akaingiwa na roho ya shetani akaanza kutamani waume za watu jirani na walikokuwa wakiishi.

> **Mume wake alikuwa mtu wa safari, hivyo mwanamke kupata mwanya wa kuzurura. Mume alipogundua, akatengana naye na kuchukua watoto wake, ili awasomeshe kwani mke hakuwa na kazi.**

Mume wake alikuwa mtu wa safari, hivyo mwanamke kupata mwanya wa kuzurura. Mume alipogundua, akatengana naye na kuchukua watoto wake, ili awasomeshe kwani mke hakuwa na kazi.

Bibie akawa wa kuzurura akakutana na baba mmoja aliyedai ni wa Msumbiji wakapendana na kumuahidi kumuoa, kwani mkewe alishafariki muda mrefu. Akamkatia pasipoti wakaondoka Msumbiji.

Baada ya miezi sita bibie akarejea nchini na tayari alikuwa mjamzito. Akajifungua mtoto wa kiume huku akiwasiliana na yule bwana. Mtoto alipofikia miaka mitatu, bwana akamwambia anamchukua akamwanzishie shule nzuri Msumbiji, bibie akakubali.

Tangu wakati huo jamaa hakuwasiliana tena na bibie akatokomea na mtoto huyo hadi leo. Kwa mume wa kwanza alizaa watoto wawili wakachukuliwa na baba yao, kisha akazaa mtoto mmoja na mwanaume mwingine naye akatokomea na mtoto wake. Amebaki mwenyewe akizurura tu.

Msomaji wangu usipokuwa makini na kumrudia Mungu, dunia inaweza kukuyumbisha hadi uone kitanzi mbele yako. Swali linakuja, unayetaka akuoe unamjua? Kama ulitumia akili zako mwenyewe kumtafuta mume pasipo kumshirikisha Mungu, majuto ni yako mwenyewe usimlaumu mtu.

Watu wenye sekeseke za aina hii wapo wengi na pengine hawajui chimbuko la yale wanayokutana nayo katika maisha yao. Lazima ujiulize umekulia kwenye misingi ya aina gani. Je, wazazi wako walikuwa na maisha ya kuoa na kuacha? Au walioa wake wengi au mama aliolewa na mwanaume zaidi ya mmoja?

Yuko mwanawake anadanganywa na mtu kwamba nilishamuacha mke wangu tukagawana vyote ila nasomesha tu wanangu. Kumbe ni mwongo anataka tu kujirusha nawe, kwa sababu fedha zinamruhusu.

Wanaume wengine wamekubali hata kwenda kutambulishwa kwa wakwe wapya kwamba wapo tayari kuoa kumbe ni geresha tu. Huyu anaye mke kwao na wala hawajaachana anacheza na fedha zake. Hii ni hatari sana.

Ulaghai huu hufanywa sana na wanaume wafanyabiashara toka baadhi ya nchi za nje. Mama mmoja aliishia kujuta pale alipompata baba mmoja mfanyabiashara mkubwa toka Afrika Kusini, wakakubaliana kuoana.

Mama huyu ana watoto wawili na baba watoto kadhaa. Mwanaume akamwambia walishaachana na mkewe kitambo hivyo angependa waoane waishi pamoja. Mwanamke akamtambulisha kwa ndugu.

Iko siku wamekaa sehemu, simu ya mwanaume ikaita akaipokea. Kumbe alikuwa ni mkewe ambaye wanaishi wote huko Afrika Kusini. Baba akawa anaongea kwa kujihami huku akimwambia nilishakwambia tuma ujumbe siyo kupiga simu. Akamkatia simu mkewe.

Baada ya hapo ukazuka mzozo mkubwa. Kumbe jamaa alitaka tu mwanamke wa kuwa naye wakati akiwa safarini kikazi na siyo mwanamke wa kuoa kama alivyomuwaminisha bibie. Maisha Ndivyo Yalivyo.

Wengi wanateseka katika ndoa, kwa sababu hawarudi kwenye chimbuko lao kabla hawajachukua maamuzi ya kuoa au kuolewa. Hawamshirikishi Mungu. Kama Mungu ndiye aliyempa Adamu mke, kwa nini asikupe na wewe ukimuomba?

Mwambie Mungu; kama vile ulivyompa Adamu mke nipe na mimi. Kumbuka mume mwema au mke mwema ni hatua ya maisha yako! Mwambie Mungu akufunulie siri ya maisha yako.

Chunguza maisha ya wazazi wako utagundua roho ya mitala (wake wengi). Hawatulii na mke/mume mmoja. Jiheshimu Mungu akupe mwenza sahihi kutimiza ndoto za maisha yako!

***Niishie hapa. Una maoni? Ujumbe 0715268581. Namba hii ipo WhatsApp.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi

# Wajasiriamali wa imani, wajasiriadini au mitume?

YAKO maswali watu wa kawaida wasio haki katika imani wanajiuliza. Kwa nini wanatoza watu fedha, ili kuwaombea? Kwa nini utajiri wa kufuru? Kwa nini sasa ni lazima kwanza ununue mafuta au maji ya upako?

Watu wengi wakifikiri ujasiriamali ni kuwa na biashara fulani ya kuingiza kipato au kufanya shughuli ya kujiajiri kwa namna fulani.

Ngoja nikumegee siri ya hawa wajasiriamali wa imani kwa maneno mengine wajasiriadini. Hawa ni watu wenye maarifa makubwa, karma.

Wao wanajua kabisa ujasiriamali ni kuwa jasiri, ili upate mali na ndio maana wanatumia nguvu nyingi za ushawishi, kuuza bidhaa zao, wajipate kiuchumi.

Mali si lazima kuwa na utajiri mkubwa, ila hali ya kubadili maisha kwenda hatua nyingine bora kuliko ya awali. Msingi wa kufanya hivyo si kuwa na mtaji wa pesa, ila mtaji wa kutosha wa ujasiri.

Biashara haiangalii unaamini kupitia nini. Biashara haiangalii wewe ni mkristo, mwislamu, mpagani au mhindu. Kuna imani ambazo biashara inakutengenezea na inataka ufanikiwe kupitia hizo.

Kwa hiyo, ili kufanikiwa katika biashara yako, unatakiwa upitie. Ukipishana nazo, lazima matokeo yake hayatakuwa mazuri.

Sikatai kuwa hakuna manabii lakini Biblia imeonya kuwa nao makini sana, kwa sababu kuna manabii wa uongo na Biblia imethibitisha hilo. Hawa si manabii wa Mungu bali ni manabii wa shetani.

Mfano, nabii anasema kuna mtu hapa anaumwa kichwa aje mbele. Huyo si nabii maana Mungu hababahatishi, nabii wa Mungu anakutaja moja kwa moja bila kubahatisha.

Ukiona nabii anahubiri mafanikio sana badala ya kuonya, jua unapigwa. Utakuta nabii anahubiri mafanikio ya kiuchumi, magonjwa na matatizo, fahamu anatafuta kuwateka, kwani ndiyo mahitaji yetu wanadamu na Mungu analijua hilo.

Mathalani, mafuta na maji ya upako yamekuwa yakinifikirisha sana, si kwamba natafuta kiki au nina nia ovu ya kuharibu taswira ya kazi za kitumishi kiimani, lahasha!

Kimsingi, ninachokifanya ni kusema ukweli kwa mtazamo wangu wa kidunia, ili mtu afanye chaguo sahihi bila kudanganywa.

Tatizo langu haliko kwenye mafuta wala maji bali kwa wale wanaoyatoa kwa kuwahadaa watu. Ninachotaka hapa kueleza ni ile nia waliyonayo ya kuwauzia wateja mafuta, wakiwaeleza kuwa ni dawa kama ilivyo Azuma na si kuhadaa watu kwa kumtaja Mungu.

Septemba 21, mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, alinukuliwa akisema Tanzania hivi sasa ina viongozi wengi wa dini, lakini si maarufu kwa neno la Mungu au uponyaji kama walivyofanya mitume.

Akaenda mbali zaidi akisema kutokana na ombwe hilo, kwake yeye kama Makonda, Mwana wa Mungu, anawatangaza ni maaskofu feki, wachungaji feki, manabii feki na mitume feki.

"Wana wa Mungu niwaambieni, ukimuona kiongozi wa dini mwenye jina lakini umaarufu wake hautokani na kazi ya mikono ya kristo, hautokani na kazi za Mungu; jua huyo ni kiongozi wa dini feki.

"Nchi yetu sasa hivi ina viongozi wengi wa dini lakini si maarufu, kwa neno la Mungu. Maarufu kweli si kwa kazi ya uponyaji kama wanavyofanya mitume. Hao mimi Makonda, Mwana wa Mungu, ninawatangaza ni maaskofu feki, ni wachungaji feki, ni manabii feki, ni mitume feki.

"Yaani hii kofia ya ukuu wa mkoa, kuna wakati mimi nawaza nasema eeh Mungu wangu eeh, sijui ningechomoka kidogo ningekaa huku nihangaike na neno? na watu ni waoga," anabainisha.

Kuna lile kanisa sijui kiboko ya wachawi, mara serikali imemtimua nchini, mara anaombea watu mpaka ulipe pesa na mambo mengine kama hayo. Tuamke tujifunze kufanya utafiti kwanza. Tunadanganywa ndugu zangu.

Nakushtua tu kijanja, mchunguze kwanza huyo nabii kwa taarifa ndipo uende. Kama utajipeleka utahamishiwa magonjwa, ili wakuombee kinafiki alafu wajitukuze wao.

Kama ndivyo, sijakosea kuwaona manabii na mitume wa aina hii kama wajasiriamali wa imani.

***• Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# HARUSI









Ilikuwa siku ya furaha na kukumbukwa kwa Peter Nyangei Mwita, baada ya kufunga ndoa na mkewe kipenzi. Sherehe hiyo ilifanyika jijini Mwanza hivi karibuni. PICHA: MC Salagata.

MITINDO

# Tupia Jeans ya kuchanika

KUNA mitazamo tofauti ya watu kuhusu vazi la jeans la kuchanika maarufu kama 'Crazy Jeans'. Wapo wanaona nguo za aina hiyo ni za kihuni, lakini wapo wanaoamini kwamba ni moja ya mtindo wa kisasa.

Kutokana na maoni hayo mchanganyiko, bado nguo hizo zinazidi kujiongezea umaarufu hasa kwa vijana wanaopenda kuvaa nguo za kipekee.

Hata hivyo, ukweli unabaki kuwa Jeans za kuchanika ni moja ya nguo zinazonunuliwa kwa wingi katika soko la mitindo duniani.

Baadhi ya watu wanaopenda kuvaa Jeans za aina hiyo wanasema, zinaleta mwonekano wa kipekee na mvuto uliokamilika hasa kwa vijana wa kiume.

Jeans za kuchanika zina sifa za kuendana na aina mbalimbali za nguo na viatu.

Ukivaa suruali au kaptula ya Jeans ya kuchanika inapendeza ukivaa juu fulana, shati la kubana au sweta.

Unapotaka viatu, hauna shida pale utakapovaa viatu aina ya raba, buti, sandozi au viatu vingine vya wazi.







## UREMBO
Na Mary Geofrey



# Unawezaje kuwa na ngozi laini?

KILA mtu hususani mwanamke anapenda kuwa na ngozi laini ya mwili na isiyo na mikwaruzo.

Ngozi laini huongeza mvuto wa mwili pamoja na mng'aro wa kipekee.

Ulaini wa ngozi hupotezwa na mambo mbalimbali, kama vile kupungukiwa maji na seli za ngozi na kusinyaa, kujeruhiwa na kufa.

Matokeo yake ni ngozi kuwa michirizi, makunyanzi, makovu, chunusi, madoa, ngozi kufubaa na kuzeeka.

Pia ngozi kuwa laini unahitaji mwili kuwa na virutubisho vyote na kunywa maji ya kutosha, ili seli zisikauke, kusinyaa wala kunyauka. Kula mlo kamili, matunda mengi na kunywa maji ya kutosha.

### JUA
Epuka jua kali ambalo litaunguza ngozi, kuikausha na kuifanya iwe na makunyanzi na vitu vingine vinavyoota kwenye ngozi kutokana na jua.

### VIPODOZI
Kwa kiingereza vinaitwa "Moisturizers", hivi hufanya kazi ya kufunika ngozi na kuzuia maji yasipotee kutoka kwenye ngozi na pia husaidia kuongeza maji kuingia kwenye seli za ngozi. Vipo katika mtindo wa sabuni, mafuta na losheni.

### VIPODOZI VYA KUZALISHA SELI
Hivi husaidia kuzalisha seli mpya za ngozi, ambazo zitaleta ngozi mpya na nzuri na kuondoa ile ya zamani iliyochoka na kuzeeka. Mfano ni losheni na krimu zenye Vitamini A na Vitamini E.

### VIPODOZI VYA KUONDOA UCHAFU
Tumia sabuni zenye uwezo wa kuondoa uchafu kutoka kwenye ngozi na ukiweza tumia 'face wash' au 'facial cleansers'. Hivi husaidia kusafisha kabisa ngozi na kuondoa uchafu.

## MAPISHI

# Mtori chakula chenye faida mwilini



CHAKULA cha mtori ni maarufu nchini na kinachotumika wakati wa asubuhi na watu wazima au watoto.

Chakula hiki kinaliwa huku kikisindikizwa na vitafunwa mbalimbali kama chapati na maandazi.

Kwa watoto wadogo, wagonjwa na mama wazazi waliotoka kujifungua, chakula hiki kimekuwa sehemu ya mlo wao wa kila siku, kwa ajili ya kuwaongezea nguvu.

Kuna aina mbalimbali za mapishi ya chakula hiki. Mapishi ya mtori kwa kutumia kipekecho (kifaa cha asili kinacho tumika kusaga chakula), blenda au kusaga na mwiko.

Leo tutajifunza aina hizo tatu rahisi ambazo unaweza kupika nyumbani na ukaachana na habari ya kununua mgahawani au hotelini. Mara baada ya nyama na ndizi kuiva anza kwa kuweka ndizi kwenye bakuli safi au sufuria, kisha uziponde ndizi kwa kipekecho taratibu na kuondoa mabonge yote.

Baada ya hapo, anza kusaga kwa kupekecha taratibu huku unaongeza supu ya nyama taratibu mpaka ndizi zako zilainike kabisa.

Rudia hatua hiyo mpaka uridhishwe na ulaini wa mtori wako, kisha rudisha jikoni ongeza supu iliyobaki, mafuta ya kupikia, chumvi, kitunguu, karoti hoho na uache uive kwa dakika tano na mtori wako utakuwa tayari.

### Kusaga na blenda
Aina hii ya mapishi inafaa sana kwa watu wenye haraka, unachotakiwa kufanya ni kuweka ndizi zako zilizoiva kwenye blenda, ongeza supu na usage mpaka zilainike.

Hakikisha ndizi zako zimepoa ndipo usage pia uweke kidogo kidogo, ikiwa una ndizi nyingi.

Baada ya hapo mimina mchanganyiko wako kwenye sufuria ongeza supu iliyobaki, mafuta ya kupikia kiasi, chumvi, kitunguu, karoti hoho na uache uive kwa dakika tano na mtori wako utakuwa tayari kwa kuliwa.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Panga stoo ufukuze panya

LEO tuangazie chumba chetu cha kuhifadhia vitu, stoo zetu za jikoni. Chumba hiki kisipotunzwa vizuri kinageuka kuwa kichaka cha mende, panya na wadudu wengine.

Niseme tu kwamba mpangilio na usafi utaiweka stoo yako kwenye kiwango kizuri mwaka mzima, hata kama hauna shelfu au makabati.

Wataalamu wa mapambo ya ndani wanaeleza kuwa, watu wengi wanajisahau kwa upande wa stoo za jikoni, jambo linalosababisha isiwe sehemu nzuri ya kuhifadhi vitu, hususani vyakula badala yake panakuwa 'jalala' la ndani.

Wanaeleza kuwa stoo zilizogeuka jalala hazina mpangilio na hivyo baadhi ya vitu vinasahaulika.

"Mpangilio ni kiini cha usafi ndani ya nyumba na hasa stoo. Utakapoweza kupangilia utakuwa umejikomboa jumla," anasema Joyce Boaz.

"Unatakiwa kuweka vyakula kwenye makopo yanayoonesha ndani, kama ni ya kioo au plastiki, kama huna aina hiyo weka lebo, ili utakapotaka kutumia iwe ni rahisi kujua nini uchukue na urudishe kiurahisi," anafafanua.

Anasema stoo ni sehemu ambayo vitu vyote vinapaswa kuonekana "siyo sehemu ya kutafuta vitu."

Anashauri kuwa vitu vizito kama ndoo za nafaka vinatakiwa viwekwe shelfu za chini na vyepesi kama viungo vikae juu.

Joyce anasema vyombo visivyotumika mara kwa mara vifungwe vizuri, ili kuzuia kuharibika.

Anasema katika mpangilio, vyakula visiwekwe pamoja na vifaa vingine kama sabuni.





# Fanya ubunifu bora wakati wa ujenzi wa nyumba

KAMA ilivyo kwa viumbe hai kuathiriwa na mazingira wanayoishi, ndivyo ilivyo pia kwa viumbe visivyo hai, ikiwamo nyumba.

Ili kuepuka majengo yasiathirike, ni vyema ubunifu wake ufanyike katika hali ya ubora wa hali ya juu katika sehemu husika linapojengwa jengo.

Msanifu majengo, Daud Chikalo, anasema hata ujenge nyumba nzuri na kubwa kiasi gani, kama haijabuniwa na kujengwa kwa kuzingatia mazingira ya eneo husika, lazima iwe hatarini kuathirika.

Chikalo anasema kabla ya kuanza kujenga nyumba ni lazima ufanye uchunguzi katika eneo husika kubaini endapo kuna magonjwa yanayoweza kuathiri nyumba yako na kufanya ubunifu wa kukabiliana nayo.

Mtaalam huyo anasema endapo nyumba hiyo itajengwa pasipo kufanyiwa ubunifu mzuri huenda ikaathiriwa na magonjwa hayo.

Anasema miongoni mwa magonjwa yanayoathiri nyumba endapo haijafanyiwa ubunifu mzuri ni kutitia. Anasema mara nyingi hutitia kutokana na aina tofauti za udongo, kiwanja au kimo cha msawazo wa msingi kuwa tofauti pamoja na ubunifu hafifu wa udongo kulingana na uzito wa jengo husika.

Ugonjwa mwingine anasema ni nyumba kupitisha maji, na kwamba maeneo mengi ya Tanzania, yamezungukwa na vyanzo vya maji na yanahitaji usanifu na ubunifu wa hali ya juu wakati wa ujenzi wa nyumba, ili kuepuka athari baadae.

"Maeneo mengi ya pwani majengo yake mengi yameathiriwa na tatizo hili na hata limekuwa kero kwa wakazi na watumiaji wa majengo hayo. Baadhi ya majengo yanapitisha maji kwa njia ya sakafu na kuta mithili ya chujio au chemchem na mara nyingi utagundua kwa kuona ardhi yake inatoa maji wakati wote wa majira ya mwaka.


"Majengo mengi ya maeneo haya yanaoza na kutitia kwa haraka na hata mashimo ya vyoo vyake huinuka kwenda juu ambalo ni hatari kwa afya za wakazi. Katika hali hii kuta na sakafu huoza kwa haraka kutokana na maji yaliyoko chini ya ardhi, kuwa na kemikali mbalimbali zilizoko kwenye maji hayo. Kwa hiyo katika mazingira haya lazima yatumie malighafi sahihi za kuzuia maji hasa wakati wa ujenzi," anasema.

Lingine, anasema ni kuoza kwa nyumba na kwamba hali hiyo hutokana na unyevunyevu na kemikali mbalimbali kupitia maji kukaa kwa muda mrefu kwenye kuta na kuathiri ubora wa kuta hizo.

"Na hii husababisha kumea kwa mimea ambayo husababisha ukungu wa kijani, kwenye kuta ambao huzalisha fangasi mbalimbali wanaokula kuta," anasema.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
NINGEKUJA MWANZONI LAKINI WAIFU MZEMBE HAJA-NIKUMBUSHA ATANIKOMA!
ANDIKA UTOKE BHANA!
NIMEUSAHAU MWAKA WANGU
WAPI?
JIANDIKISHE
MWISHO LEO
LOH!
MBONA FOLENI HAIENDI
TOKENI NITAJE MWAKA
MECHI YA WATANI 'NIMEBETI' NIMEKULA MAMILIONI TAYARI
KWA HIYO NIKAKUPUMZISHE SERO UPANGE BAJETI?
KITUO CHA BASI
MIMI SIO CHANGUDOA SITAKI
NDIO MWAMBIE WE' 'PROSTUTA'
UTANI WA WATANI ULISHAISHAGA JANA
KWANI NGAPI NGAPI HAPO TU
MUDA UMEISHA TUNAFUNGA BAR
HELA HAIJAISHA KANIFUNGIENI KAUNTA MKALALE
BAR

HABARI KIMATAIFA

# Viongozi wa upinzani wauawa Msumbiji

**MAPUTO,** MASUMBUJI

WATU wenye silaha wamemuua mwanasheria na ofisa wa chama cha upinzani nchini Msumbiji, baada ya kulifyatulia risasi gari walilokuwa wakisafiria.

Tukio hilo limetokea jana, limeongeza hali ya wasiwasi kabla ya kufanyika kwa maandamano ya kupinga matokeo ya uchaguzi.

Kundi la waangalizi wa uchaguzi kutoka mashirika ya kiraia nchini humo, linalojulikana kama More Integrity, lilisema shambulio hilo lilitokea katika kitongoji cha Bairro Da Coop katika mji mkuu Maputo.

Waliouawa ni wakili wa Podemos Elvino Dias na mwakilishi wa chama hicho, Paulo Guambe.

"Waliuawa katika mauaji ya kinyama," alisema Adriano ambaye ni mkurugenzi wa Kituo cha Demokrasia na Haki za Kibinadamu cha Msumbiji (CDD).

Chama kipya cha upinzani cha Podemos, ambacho mgombea wake wa urais Venancio Mondlane, kimepinga matokeo ushindi chama cha FRELIMO, kilichotawala Msumbiji kwa nusu karne.

Kambi ya upinzani wapanga kuitisha maandamano nchini kote kuanzia kesho.

**BBC**

# BRICS kukuza uchumi wa dunia

**MOSCOW,** RUSSIA

RAIS wa Russia, Vladmir Putin, amesema kundi la nchi za BRICS, litachangia ukuaji wa uchumi duniani katika miaka ijayo, kutokana na ukubwa na ukuaji wake.

Putin alisema nchi zinazounda kundi hilo zinashamiri kiuchumi ukilinganisha na ule wa mataifa yaliyoendelea ya Magharibi.

Alisema anatumaini BRICS inazidi kutanuka na kuzijumuisha Misri, Ethiopia, Iran na Umoja wa Falme za Kiarabu (U.A.E).

Nchi zinazounda kundi hilo ni Brazil, Russia, India, China na Afrika Kusini.

Kiongozi huyo atakuwa mwenyeji wa mkutano wa kilele wa BRICS utakaofanyika katika mji wa Kazan, kuanzia Oktoba 22 hadi 24, mwaka huu.

**DW**

# Cuba gizani baada ya mtambo kuzima

**HAVANA,** CUBA

imekuwa gizani baada ya kuCUBA imekuwa gizani baada ya kukatika kwa umeme nchi nzima, baada ya moja ya mtambo mkuu wa kuzalisha kushindwa kufanya kazi na kusababisha gridi ya taifa kuzimwa.

Katika kubana matumizi ya nishati hiyo, serikali iliamuru kuzifunga shule na taasisi zingine pamoja na kuwaamuru wafanyakazi wa serikali kurudi nyumbani,

Wizara ya Nishati nchini humo ilisema katika taarifa yake kuwa, kituo cha kuzalisha umeme cha Antonio Guiteras, ambacho ni kikubwa zaidi na chenye ufanisi kilizima na kusababisha hitilafu kwenye gridi ya taifa.

Kutokana na tatizo hilo, watu zaidi ya milioni 10 wamekosa nishati ya umeme.

Hata hivyo, haikuelezwa ni nini kimesababisha mtambo huo kuzima.

Kisiwa hicho kinachopakana na Marekani, kinakabiliwa na hali mbaya ya kiuchumi, wakazi hawana chakula cha kutosha, mafuta, maji na dawa. Rais wa Cuba, Miguel Diaz-Canel, alisema kupitia mtandao wa X kwamba watafanya kila wawezalo kurejesha nishati hiyo.

Tatizo la kukatika kwa umeme limesababisha serikali kufuta huduma zote zisizo na muhimu, kuanzia Ijumaa ya wiki hii.

Waziri Mkuu, Manuel Marrero, alisema kuwa tatizo la kukatika kwa umeme liloanza wiki kadhaa zilizopita, limechangiwa zaidi na dhoruba, kuzorota kwa miundombinu, uhaba wa mafuta na kuongezeka kwa mahitaji.

"Uhaba wa mafuta ni sababu kubwa", alisema Marrero katika ujumbe kwa taifa kwa njia ya televisheni.

Maofisa wa serikali walisema upepo mkali uliotokana na kimbunga Milton kilichoipiga Marekani wiki iliyopita, kimesababisha ugumu wa kusambaza mafuta kutoka katika meli zilizotia nanga nje ya nchi, kwa ajili ya kupeleka kwenye mitambo yake ya kuzalisha umeme.

**DW**



Baadhi ya wakazi wa jiji la Havana, wakiwa nje ya makazi yao wakipunga upepo baada ya nchi hiyo kukosa umeme kwa siku kadhaa.. **PICHA: AFP**

# Hezbollah yashambulia nyumba ya Netanyau

**TEL AVIV,** ISRAEL

NDEGE isiyo na rubani iliyorushwa na kundi la Hezbollah, ilifanikiwa kupenya na kuilenga nyumba ya Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu.

Nyumba ya kiongozi huyo, iko katika mji wa Caesarea kaskazini mwa Israel ambayo inalindwa vikali na jeshi la nchi hiyo.

Msemaji wa Netanyau, alisema tukio hilo lilitokea jana, lakini kiongozi huyo hakuwapo katika jengo hilo na hakuna mtu aliyejeruhiwa.

Hata hivyo, Jeshi la Israel lilisema ndege tatu zisizo na rubani zilirushwa kuelekea mji huo, ulioko pwani na moja iligonga jengo hilo na mbili zilidunguliwa kabla ya kulipuka.

Serikali ya Israel haijasema chochote kama jengo hilo lilikuwa sehemu ya makazi ya Waziri Mkuu, wala kiwango cha uharibifu.

Netanyahu anatumia nyumba mbili katika miji ya Kaisaria na Jerusalem na wakati mwingine anatumia muda wake katika mji wa Beit Aghion, ambako kuna makazi rasmi ya waziri huyo ambayo kwa sasa inafanyiwa ukarabati.

Jeshi lilisema jumla ya roketi 55 zilirushwa kuelekea Israel kutoka Lebanon, kwa siku ya jana pekee.

Wakati huo huo, Kiongozi Mkuu wa Iran, Ayatollah Ali Khamenei, alisema kundi la Hamas litabaki kuwa hai licha ya kifo cha kiongozi wake, Yahya Sinwar.

Sinwar, anayedaiwa kuwa mhusika mkuu wa mashambulizi ya Oktoba 7 mwka jana, dhidi ya Israel, aliuawa baada ya wanajeshi wa Israel kushambulia jengo moja mjini Rafah, mapema wiki hii.

"Kifo chake bila shaka ni pigo kubwa, lakini harakati za kupigania haki hazitafifia licha ya mauaji ya watu mashuhuri," alisema Khamenei katika taarifa yake.

Katika matukio mengine, watu 33 wameuawa na wengine 85 wamejeruhiwa katika mashambulizi ya anga yaliyofanywa na Israel katika kambi ya wakimbizi ya Jabalia kaskazini mwa Gaza, usiku wa Ijumaa.

Mamlaka inayoongozwa na kundi hilo la Hamas, ilisema idadi ya vifo huenda ikafikia 50, kutokana na watu wengine hawajafikiwa kutokana na kuangukiwa na vifusi.

Vikosi vya Israel vimeizingira kambi hiyo yenye wakazi wengi kwa wiki kadhaa, vikisema mashambulizi yake huko yanalenga kuwazuia wapiganaji wa Hamas kujipanga upya, ili kufanya mashambulizi zaidi.

Takriban watu 400,000 wapo ndani ya kambi hiyo wakiwa hawana chakula na maji kwa zaidi ya wiki mbili.

Mapigano pia yanaendelea nchini Lebanon, wakati Israel ikifanya uvamizi wa ardhini dhidi ya kundi ya Hezbollah.

Jeshi la Israel lilisema kuwa, limewauwa wapiganaji 60 wa Hezbollah na kuharibu kituo cha mawasiliano cha kikanda cha kundi hilo linaloungwa mkono na Iran.

**BBC**

# Mwinyi aagiza taasisi za elimu kuanzisha kozi zenye uhitaji wa wataalamu wa afya

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amezishauri taasisi za elimu ya juu nchini, kuanzisha kozi muhimu zenye uhitaji na uhaba wa wataalamu zitakazochangia maendeleo ya nchi.

Dk. Mwinyi amesema hatua hiyo itaisaidia sekta ya afya kuwa na wataalamu wa kutosha katika kada mbalimbali watakaotoa huduma kwa kuzingatia utaalamu na weledi na kuimarisha sekta hiyo.

Rais Dk. Mwinyi alisema hayo jana katika viwanja vya Mao Tse Tung, kwenye Mahafali ya 12 ya Chuo cha Afya Zanzibar (ZSH).

Pia alitoa wito kwa wahitimu wa kada tofauti kuzingatia nidhamu na maadili ya kazi katika utoaji wa huduma wanapoingia kwenye majukumu yao na kuwa msaada muhimu kwa jamii.

Dk. Mwinyi pia aliwasisitiza vijana kusoma kozi zenye umuhimu na uhitaji hususani mpya zinazoanzishwa na ZSH na kupongeza juhudi zinazochukuliwa na chuo hicho kuanzisha kozi mpya.

Aidha, aliwahakikishia wamiliki kuwa serikali itaendelea kuunga mkono malengo ya chuo hicho ya utoaji wa taaluma bora na juhudi ya kuelekea kuwa chuo kikuu cha afya nchini.

Rais Mwinyi alisema juhudi hizo zinaendana na malengo ya serikali ya kuona chuo hicho kinakuwa chemchem ya kuzalisha wataalamu katika sekta afya.

Dk. Mwinyi alitoa wito kwa wahitimu kutoridhika na elimu waliyoipata bali kutafuta fursa zaidi juu kuziongezea maarifa na ujuzi.

Wakati huo huo, Dk. Mwnyi alizindua stashahada ya usimamizi wa mfumo wa taarifa za afya na stashahada ya uchunguzi wa macho.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Moh'd Mussa, aliipongeza taasisi hiyo kwa kuendelea kuzalisha wataalamu wa kada mbalimbali katika sekta ya afya, hatua aliyosema ni muhimu kwa ustawi wa jamii na kuimarisha huduma ya afya.

Alisema hatua ya kuanzisha kozi mpya itaisadia nchi kuwa na wataalamu wa kutosha katika kada tofauti na kuahidi kwa wizara kuunga mkono.

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa ZSH, Aziza Omar Hemedi, alisema wahitimu wa chuo hicho wamekuwa nguzo muhimu ya utoaji wa huduma za afya katika vituo vya afya kwa wananchi.

Alisema chuo hicho kimeanzisha kozi mpya tatu za stashahada ya usimamizi wa majanga, stashahada ya uchunguzi wa macho na stashahada ya ushauri nasihi.

Wahitimu 640 wa kada mbalimbali wamehitimu na kutunukiwa vyeti na Rais Dk. Mwinyi. Chuo hicho tangu kuanzishwa mwaka 2011, kimezalisha wahitimu 3,000 ambao wametawanyika kwenye taasisi mbalimbali za umma na binafsi, kwa ajili ya kutoa huduma.




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akiwatunuku wahitimu wa stashahada mbalimbali wakati wa mahafali ya 12 ya Shule ya Afya Zanzibar katika Uwanja wa Mao Tse Tung, Wilaya ya Mjini Unguja, jijini Zanzibar jana. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shule hiyo, Aziza Omar Hemed. **PICHA: IKULU**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Haruna aliyesingiziwa kumroga mtoto wa kaka



**Na Adam Fungamwango**

**Leo tutauangalia wimbo wenye maudhui hayo, uliopigwa na Orchestra Safari Sound (OSS), iliyokuwa chini ya Kikumbi Mwanza Mpango, King Kiki, mwanzoni mwa miaka ya 1980, uliotwao, 'Haruna Kaka.'**

HIVI karibuni tumekuwa tukisikia kwenye vyombo vya habari, kukamatwa na baadhi ya waganga wa kienyeji wakiwa na mabaki ya miili ya watu.

Haijulikani waliyapata wapi, waliwaua na kuchukua mabaki na viungo hivyo au walinunua.

Jeshi la Polisi likaonya waganga wote wenye tabia ya ramli chonganishi. Hizi ni tabia za baadhi ya waganga ambao badala ya kuwatibu wateja wao, huwaambia na watu ambao wamewafanyia mabaya.

Bahati mbaya wanaotajwa wengine wa baba, mama, watoto, shangazi na ndugu wengine wa karibu wa mteja.

Hali hii imekuwa ikileta uhasama na mfarakano mkubwa kwenye familia na jamii kwa ujumla.

Watu wanakasirikiana, wananuniana, hawatembeleani, wanaogopana, kisa mganga.

Pamoja na baadhi ya waganga kuwa na tabia hiyo, lakini pia baadhi ya watu wamekuwa wakiamini mno mambo ya kishirikina.

Akiumwa hata mafua basi yeye anaona amerogwa. Akitaka kufanya kitu chochote ni lazima aende kwa mganga wa kienyeji kwanza.

Hali hii imekuwa ikiwaumiza watu wengi hasa barani Afrika, ambako ndiko kuna watu wengi wenye imani hizo.

Akitaka kazi, mtoto, asikamatwe, adumu kwenye ndoa, au kutaka mke au mume, ni lazima kwanza aonane na mganga.

Baadhi ya Waafrika wanaamini zaidi nguvu za waganga kuliko hata uwezo, elimu au vipaji vyao.

Afadhali miaka ya nyuma unaweza kusema watu wengi walikuwa kwenye zama za giza, yaani walikuwa hawajaendelea kwa kusoma na kupata elimu, lakini cha ajabu hata leo karne ya 21, pamoja na kupata elimu kubwa na maendeleo ya teknolojia, bado watu wanaamini nguvu za giza, yaani uchawi.

Tena naweza kusema karne hii, ndiyo watu wanaamini zaidi kuliko hata miaka ya nyuma. Kwa sababu kipindi hicho wengi walikuwa hawana elimu na uelewa na kutosha, lakini baadhi yao walipopata wakaachana na mambo hayo.

Utashangaa leo, kuna elimu ya kufahamu kwa nini mtu anaumwa na akiumwa kitu fulani kinatokana na ukosefu wa kitu fulani na nini anatakiwa kufanya, bado anaamini kwenye mambo ya ulozi.

Leo tutauangalia wimbo wenye maudhui hayo, uliopigwa na Orchestra Safari Sound (OSS), iliyokuwa chini ya Kikumbi Mwanza Mpango, King Kiki, mwanzoni mwa miaka ya 1980, uliotwao, 'Haruna Kaka.'

Ikiwa kwenye mtindo wa 'Masantula Ngoma ya Mpwita', bendi hiyo ilipata sifa kubwa na kujinyakulia mashabiki lukuki.

Maudhui ya wimbo huo ni kwamba, mtoto wa jamaa mmoja alikuwa anaumwa. Anachouwa hakijulikani kwa sababu hajampeleka hospitali. Kwa kuamini mambo ya Kalumanzira, akaenda kwa mganga wa kienyeji, aliambiwa kaka yake ndiye aliyemroga mtoto huyo. Ilikuwa ramli chonganishi kwani jamaa alimjia juu kaka yake kumwambia ni mchawi. Pamoja na hayo, kaka mtu hakuja juu, badala yake alimshauri mdogo wake, wampeleke hospitali akafanyiwe vipimo, mtoto hajarogwa na wala yeye si mchawi.

Wimbo huu ulikuwa maarufu sana enzi hizo, unaanza na mashairi kama ifuatavyo.

"Haruna ee, Haruna nimekuja kukueleza sisi ni wandugu mbona kelele. Mtoto wa kwako pia ni wa kwangu Haruna yashangaza. Nimefika kwa waganga kuulizia, wamekugundua. Nimekuja kukueleza tushauriane kisa gani tukosane we nami?

Yanitia uchungu kwa hiki kitendo, kwa hiki kitendo kimefanyika, naomba tuelewane.

Hakuna kaka, Haruna kaka Haruka Haruna kaka, Haruna kaka, Haruna kaka."

Jamaa analalamika, akimtuhumu ndugu yake kuwa amemfanyia kitendo kibaya mtoto wake na hayo ameyapata kwa mganga wa kienyeji.

"Mimi wenu kweli napatikana, kweli napatikana shauri ya wangu, shauri ya wangu wangu mtoto, leo kuteseka kesho kuteseka, namaliza mitaani kuulizia, kuulizia kweli waganga, kweli waganga nipate kujua, nipate kujua kisa cha magonjwa, kisa cha magonjwa cha wangu mtoto, yeyee Haruna wewe na mimi baba, ooh Haruna wewe na mimi kaka, pana makubwa."

Bado anaendelea kulalamika, na mwishoni akaamua kumfuata na kumueleza 'laivu' kuhusu jambo hilo.

Kiki na Kabeya Badu ndiyo wanazungumza kwa kujibishana kwenye wimbo huo kama mtu na kaka yake. Kiki alikuwa kama yule jamaa anayeamini uchawi, na Kabeya ni kaka mtu.

**Kiki:** Kaka Haruna nimekuja.
**Kabeya:** Eeeh nakusikia ndugu yangu eleza.
**Kiki:** Natoka Bagamoyo.
**Kabeya:** Bagamoyo? Kuna nini?
**Kiki:** Pana makubwa.
**Kabeya:** Makubwa gani tena?
**Kiki:** Watoto watamalizika.
**Kabeya:** Watamalizika na nini?
**Kiki:** Wanasema wamekugundua.
**Kabeya:** Huyo mganga wa Bagamoyo Tshilumbu amekudanganya. Amekwambia mambo ya uongo.
**Kiki:** Hapana, ameniambia ukweli.
**Kabeya:** Nakwambia kweli, amekudanganya.
**Kiki:** Sema nisikie sasa, ukweli ni upi?
**Kabeya:** Mtoto anaumwa kidonda tumbo.
**Kiki:** Sasa tufanye nini.
**Kabeya:** Tumpeleka hospitalini
**Kiki:** Tumpeleke hospitalini?
**Kabeya:** Ndiyo tumpeleke hospitali, atapona.

Muafaka wa ndugu wawili ukapatikana, mtoto akapelekwa hospitali, akafanyika vipimo, akapatiwa matibabu, akapona, ugomvi ukaisha. Wimbo huu unatukumbusha kuwa makini na ramli chonganishi kutoka kwa waganga wa kienyeji na hata kauli chonganishi kutoka kwa watu ambao wanajifanya ni watu wa Mungu, lakini kazi zao hazitofautiani na uganga wa kienyeji.

# HADITHI

## Nyuma ya Pazia-5

TAARIFA za habari kwenye televisheni, redio, mitandao ya kijamii zinaarifu kutekwa kwa mtoto wa miaka sita, Macaire, mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule moja Mbezi Dar es Salaam. Mashuhuda wanasema alinyakuliwa na mwanamume mmoja aliyeshiba, kujaa misuli na kukimbilia kwenye gari lililokuwa pembeni mwa barabara ya Bagamoyo, Dar es salaam, ambalo mlango wake ulikuwa wazi. Wazazi wa mtoto wanapigiwa simu na watekaji wakitaka kiasi cha Sh. Milioni 15 ili wamwachie. Jeshi la Polisi linaingia kazini kumsaka au kuwasaka watekaji. Walichogundua ni kisa cha kushangaza, kusisimua ambacho utakipata utakaposoma kila aina ya nakala ya gazeti hili, ili kuupata mkasa mzima wa tukio.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

ILIKUWA ni saa nne usiku. Macky alikuwa amebeba mkoba wenye pesa. Hakuna yoyote aliyejua kama ulikuwa na kiasi cha pesa taslimu Sh. milioni 15. Alitoka nyumbani kwake Manzese Argentina na kupanda basi akashukia Magomeni Usalama. Aliambaa ambaa na barabara na baadaye kukata kushoto. Hakukuwa na watu wengi sana kama inavyokuwa mchana. Alipita maeneo ya Hospitali ya Magomeni, akapita pia Kanisa Katoliki, mita kadhaa baadaye alifika eneo la mwanzo wa bonde la Mkwajuni, kuelekea Kinondoni. Kulia kulikuwa na mteremko mkali na miti mingi kama alivyoelezwa. Alivuka barabara kwani alikuwa akitembea upande wa kushoto. Ni eneo ambalo halikuwa na mwanga wa kutosha. Taa za barabarani na giza vilishindana. Giza lilionekana kushinda mwanga kwa asilimia nyingi. Baada ya kuangalia sana aligundua kuwa kuna njia nyembamba ya mteremko mkali. Woga ulimuingia, lakini akikumbuka mtoto wake Macaire, alitengeneza ujasiri ndani ya moyo wake.

Akaamua kuteremka kwenye mteremko huo, huku akijizuia asiteleze. Na kila alipokuwa akishuka ndipo giza lilivyokuwa likishamiri.

"Ukija mpaka pale kuna njia inashuka kule chini, kuna bonde kali, shuka taratibu utakutana na njia nyembamba na miti mingi na nyumba chache, utashuka hadi sehemu ambayo ni tambarare. Utakata kulia na hatua chache tu utakutana na mti mnene zaidi kuliko yote iliyokuwa hapo. Chini ya mti ndipo utakapoacha mzigo." Ilikuwa ni sauti iliyojirudia kwenye ubongo wake, akikumbuka alivyokuwa akiambiwa na yule mtekaji kwenye simu.

Kwa bahati nzuri kila alichoambiwa kilikuwa sahihi. Mpaka mti mnene alioambiwa aliukuta.

Hata hivyo kila kilichofanyika na eneo lenyewe ilikuwa ni picha ya kutisha mno. Kwa sababu pia hakujua nini kitaendelea baada ya kuweka mzigo ule ya pesa. Hakujua usalama wake kama anaweza kuwa hai. Hakujua pia usalama wa mtoto wake pale zoezi litakapofanyika. Alijua pia askari polisi watakuwa maeneo jirani wakijipanga kuwakamata au kupambana na watekaji, vinginevyo wasingempa zile pesa.

Wakati akiwa amefika kwenye mti ule ambao kwa kuutazama tu aligundua kuwa ni mbuyu, alisikia




**"Tumesitisha zoezi la kuchukua hizo pesa, kwa hiyo geuza, rudi ulikotoka, maagizo na maelekezo mengine tukakupa siku nyingine," ilisikika sauti hiyo. Tangu alipokuwa akipigia simu na watekaji, siku ile haikuwa sauti ya yule yule wa kila siku. Ilikuwa ya mtu mwingine kabisa.**

simu ikiita mfukoni. Aliingiza mkono mfukoni na kuitoa, akaangalia namba zilikuwa ngeni. Mlio mkali za simu sehemu ambayo ilikuwa kimya kama jehanamu, kulizidi kumtia hofu Macky. Haraka alibonyeza kitufe, ili ule mlio usiendelee kulia na yeyote kujua kama kuna binadamu sehemu ile.

"Tumesitisha zoezi la kuchukua hizo pesa, kwa hiyo geuza, rudi ulikotoka, maagizo na maelekezo mengine tukakupa siku nyingine," ilisikika sauti hiyo. Tangu alipokuwa akipigia simu na watekaji, siku ile haikuwa sauti ya yule yule wa kila siku. Ilikuwa ya mtu mwingine kabisa.

Kabla hajasema chochote, simu ilikatwa. Na kama kawaida, na hata alikiaribu kupiga tena mara mia, haitopatikana. Tayari walishamwambia kuwa hutumia namba moja kuwasiliana naye, na wakishamaliza hawaitumii tena, kwa sababu ya usalama wao.

Alirejea kinyumenyume na kuangalia kama kunaweza kutokea chochote, au inaweza kuwa ni mtego tu. Dakika moja baadaye aligeuka na kurudi alikotoka. Aliondoka haraka haraka kuliko alivyokuja.

Akiwa anakaribia kufika kwenye kituo cha Magomeni Hospitali, gari ambayo anaifahamu ilisimama mbele yake. Ni ile ya askari waliompa ule mkoba wa pesa kiasi cha Sh. milioni 15 ili akawape watekaji na mtoto wake aachie.

Haikuwa kwa ajili ya kuwapa, bali ulikuwa ni mtego wa polisi. Hawakumwambia chochote zaidi ya kumtaka arejeshe mkoba na kumtaka afike Makao Makuu ya Polisi Kanda, kesho mchana.

**************************************

Hakupata lepe ya usingizi. Alichojiuliza ni kitu gani kimetokea. "Ni kwa nini jamaa wamesitisha kuchukua pesa? Je usalama wa mtoto wangu upo kweli?" Akajiuliza mwenyewe.

Kulipokucha alimpigia simu mwalimu Kisanga, kumweleza tukio zima lilivyokuwa na kumtaka wakutane polisi.

Macky alifika pamoja na mzazi mwenzake Dora, mwalimu Kisanga ambao wote walikutana ndani kwa afande Chacha.

"Zoezi halijafanikiwa kwa namna ya ajabu!" Akasema afande huyo kwa kuwatazama wote kwa zamu.

"Kilichotokea ni kwamba watekaji wamegundua mchezo mzima wa jinsi tulivyojipanga kwenda kuwakatama!"

Wote watatu ndani walipigwa na butwaa. "Ni jambo la ajabu kidogo. Hili jalada lipo kwetu sisi askari watatu ambao pekee tunaojua, halafu nyinyi watatu pia. Jumla ni watu sita ambao wanajua kama kuna mpango wa kutaka kuwatia mbaroni hawa watu. Sasa kwa nini wamefahamu kuwa walikuwa wanawinda?" Akauliza afande huyo.

"Najua hamtokuwa na jibu. Na sisi kama askari polisi tunaendelea na uchunguzi wa kubaini hili. Pia tunaendelea na mpango wa kumuokoa mtoto. Hivi huwa wanakupigia kwa namba gani?" Akauliza.

Afande hawa watu ni wajanja sana, wananipigia kwa namba tofauti. Na baada ya kunipigia haipatikani tena na hata ukifuatilia unagundua kuwa ni zile ambazo hazina hata majina ya mtu aliyesajili," alijibu Macky.

"Okay! Basi tunadili na watu ambao si wa kawaida kama tulivyodhani. Hivyo inabidi tuongeze umakini. Hili jambo lisizungumzwe ovyo. Tunapotoka hapa msimwambie mtu yoyote," alisema afande Chacha na kuongeza.

"Kazi nyingine itafanywa pale watakapokupigia simu. Tukumbuke kuwa lengo la kumteka mtoto kwa jamaa hao ni pesa. Na kwa sababu hawajazipata, lakini watafute tena mbinu za kuzipata. Hawakuzichukua kwa sababu waligundua kuwa wanasakwa. Na kukuibieni siri tu, hawakuwepo hata mtu mmoja eneo ambalo walimwambia Macky aende akaweke pesa. Hii ina maana kuwa siyo kwamba walikwenda halafu wakawaona askari wetu waliokuwa wamevalia kiraia, ila hawakwenda kabisa eneo la tukio kuchukua pesa na wakakupigia simu ili arudi na hapo, ina maana walijua kabla tukio halijatokea, kitu ambacho tunajiuliza sana imekuwaje. Ila usiri unatakiwa katika hili,"akamaliza afande Chacha na kuwaruhusu wahusika kuondoka. Dora aliondoka na bajaj aliyoiita kwa njia ya mtandao na Macky alipata lifti ya mwalimu Kisanga.


**************************************

Kama ambavyo alitegemea, saa sita na nusu alisikia simu ikiita. Alitegemea simu hiyo, ingawa ilimtisha. Alikuwa bado kwenye kochi akiwa anaangalia televisheni nyumbani kwake. Hakuwa na mke, kwani tangu alipoachana na Dora, mama Macaire, miaka miwili iliyopita akili yake haijakaa sawa. Walikuja hapo ni wanawake tu na kukidhi haja zake na kuondoka. Hakutaka kabisa hata wa sogea tukae, achilia mbali kuoa.

"Wewe mpumbavu unampenda mtoto wako kweli wewe?" Ilisikika sauti ile ambayo aliizoea, siyo ya jana iliyopigwa kule bondeni Kinondoni Mkwajuni.

"Tulikwambia usiwaeleze askari polisi kuhusu wewe kupeleka pesa kule. Ilikuwa ni siri yetu wawili kweli si kweli?"

**Itaendelea Jumapili**



# ALI KIBA, RAYVANNY WAPANDISHA JOTO

MASHABIKI wa muziki wa Bongo Fleva, wameonesha furaha yao, baada ya kuonekana mastaa wawili Ali Kiba na Rayvanny, wakipika kolabo yao.

Hata hivyo haijafahamika lini wasanii hao walifanya kolabo hiyo, badala yake walionekana kwenye video iliyosambaa mitandao wakiingiza sauti ngoma yao mpya.

Baadhi ya mashabiki walielezea kuwa, wasanii hao wenye vipaji vikubwa vya muziki watatengeneza kazi nzuri na pengine inaweza kuwapiku wengine waliofanya hivyo kwa mwaka huu.

# Christian Bella hachukuliwi kama nazi

MWANAMUZIKI wa dansi, Christian Bella, amesema ni vigumu kukubali mialiko ya kazi kutoka kwa wasanii wengine, kutokana na kuwa na ratiba ya mwaka mzima.

Akizungumza hivi karibuni, Bella amesema kuna baadhi ya kazi alizotakiwa kwenda kuzifanya amezikataa kutokana na kuiingilia.

"Wasanii wezangu tuko vizuri, lakini linapokuja suala la ratiba yangu siwezi kuvunja, mfano nina kazi za mwezi Novemba na endapo atakuja mtu kuniambia ana kazi yake natakataa," amesema Bella.



## ZISIKUPITE

### MARMOUSH ANUKIA LIVER

LIVERPOOOL inavutiwa na mshambuliaji wa Eintacht Frankfurt na Timu ya Taifa ya Misri, Omar Marmoush, mwenye umri wa miaka 25. Nottingham Forest na Aston Villa zilitaka kumsajili nyota huyo msimu uliopita. ***(Sky Germany)***

### KUDUS KUWEKWA SOKONI

KLABU ya West Ham inatarajiwa kutoa bei ya kiungo wao wa kati ambaye ni raia wa Ghana, Mohammed Kudus, mwenye umri wa miaka 24. Manchester City, Liverpool, Arsenal na Chelsea zimeonesha nia ya kumsajili nyota huyo. ***(Football Insider)***

### SANE AKARIBIA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inapania kumsajili winga wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Leroy Sane, mwenye umri wa miaka 28, msimu ujao wa joto mara baada ya mkataba wake sasa wa nyota huyo utakapokamilika huko Bayern Munich. ***(Football Insider)***

### MUSIALA KUIKAMUA BAYERN

BAYERN Munich ipo tayari kumfanya Mjerumani, Jamal Musiala, kuwa mchezaji wao anayelipwa kitita kikubwa, pamoja na mshambuliaji wa Uingereza, Harry Kane, kwa paundi 400,000 kwa wiki. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 hajadokeza kufanya mazungumzo na Real Madrid au Manchester City. ***(Sky Germany)***

### O'NEIL KITAELEWEKA

KLABU ya Wolves wanadumisha uungwaji mkono wao kwa Kocha Mkuu, Gary O'Neil, 41, baada ya kumfukuza Jack Wilson. ***(Sky Sports)***

### BARCA YAMTAKA DAVID

BARCELONA inamfuatilia mshambuliaji wa Lille na Timu ya Taifa ya Canada, Jonathan David, 24. ***(Todofichajes)***

### LARSSON AGEUKA LULU

KLABU kadhaa zinamfuatilia winga wa Eintracht Frankfurt kutoka Sweden, Hugo Larsson, 20. ***(Fabrizio Romano)***

### DIBLING ATAJWA UNITED

KLABU ya Southampton inatumaini kumshawishi kiungo wa kati wa England, Tyler Dibling, 18, kusaini mkataba mpya huku Manchester United wakionesha nia ya kutaka kumnunua. ***(GiveMeSport)***

### CONNOLLY NJIA MOJA

KLABU ya Sunderland inatazamia kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Brighton na Jamhuri ya Ireland, Aaron Connolly, 24, kutoka Hull City. ***(Sun)***

### KERKEZ KUTUA ARSENAL

ARSENAL inapanga kuwasilisha dau la kumnunua beki wa kushoto wa Bournemouth na Hungary, Milos Kerkez, 20, na winga Antoine Semenyo (24), mchezaji wa kimataifa wa Ghana. ***(CaughtOffside)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI UWANJANI KLABU BINGWA YA DUNIA 2025

### ●●● Ni baada ya Inter Miami kutwaa Ngao ya Jamii...

**MIAMI,** Marekani

INTER Miami inatarajiwa kutangazwa kama mshiriki maalum wa Ligi ya Klabu Bingwa ya Dunia la FIFA (2025), kwa mujibu wa ESPN.

**Tangazo rasmi la ushiriki wa timu hiyo katika mashindano hayo, linatarajiwa kutolewa wiki ijayo.**

Ligi ya Klabu Bingwa ya Dunia itakayofanyika mwakani, itashirikisha timu 32 kutoka kote ulimwenguni kwa mara ya kwanza, baada ya FIFA kuchagua kupanua mashindano kutoka kwa muundo wake wa awali wa timu saba.

FIFA ilitoa nafasi 12 kwa Ulaya (UEFA), Amerika Kusini (CONMEBOL-sita), Amerika Kaskazini na Caribean (Concacaf- nne), Asia (AFC) na Afrika (CAF) mbili na moja kwa Oceania (OFC).

Timu nyingi zinazoshiriki tayari zimejulikana, zikiwamo Manchester City (washindi wa Ligi ya Mabingwa msimu wa 2022-23) na Real Madrid (2021-22 na 2023-24).

Monterrey (Kombe la Mabingwa wa Concacaf 2021), Seattle Sounders (Kombe la Mabingwa wa Concacaf 2022), León (Kombe la Mabingwa wa Concacaf 2023) na Pachuca (Kombe la Mabingwa wa Concacaf 2024) watawakilisha Concacaf.

Concacaf, ilipata mwaliko wa ziada kwa mashindano hayo ikizingatiwa Marekani itahudumu kama mwenyeji wa michuano hiyo.

FIFA ilihifadhi haki ya kuchagua mshiriki wa mwisho wa Concacaf, ikitoa tiketi kwa mshindi wa Ngao ya Mashabiki wa 2024 Inter Miami.

Kamishna wa Ligi ya Soka ya Marekani (MLS), Don Garber, alifichua wakati wa mchezo wa All-Star Julai 24, mwaka huu ligi hiyo inaweza tu kutoa mapendekezo kwa FIFA, lakini haitamchagua mshiriki.

Lionel Messi sasa ataongoza timu kutoka Florida Kusini katika michuano ya kimataifa itakayoanza Juni 15 hadi Julai 13, 2025 katika viwanja mbalimbali huko Marekani.




# LEWANDOWSKI KUPATA MKATABA MPYA BARCA

**BARCELONA,** Hispania

MKATABA wa straika kinara wa Barcelona, Robert Lewandowski, utaongezwa hadi Juni mwaka, 2026 ikiwa mshambuliaji huyo atafikisha asilimia 50 ya michezo klabuni hapo.

Hii ni kwa mujibu wa, Fabrizio Romano, mwandishi kinara wa habari za michezo wa Italia.

Romano amedai Rais wa Barcelona, Joan Laporta, amethibitisha kifungu hicho kuwapo katika mkataba wa Lewandowski, aliyesajiliwa kutoka kwa wababe wa Bundesliga, Bayern Munich.

Inaelezwa kocha wa kikosi cha Wakatalunya hao, Hansi Flick, amefurahishwa na kiwango cha mshambuliaji huyo ambaye mpaka sasa ni kinara wa mabao La Liga, akiwa na magoli 10.




# *Wilshere akaribia kutua Norwich*

**LONDON,** England

KIUNGO wa zamani wa England, Jack Wilshere, anatarajiwa kujiunga na Norwich City kama kocha wa kikosi cha kwanza, kwa mujibu wa ESPN.

Klabu hiyo ya Championship iko katika mazungumzo na Arsenal katika hatua ambayo itamfanya aondoke kutoka timu ya vijana chini ya umri wa miaka 18 na kuchukua nafasi ya Narcis Pelach, aliyeondoka Norwich na kujiunga na Stoke City mwezi uliopita.

Wilshere alistaafu kama mchezaji mnamo Julai, mwaka 2022, akitoa muda kwenye maisha yake ya soka aliichezea Arsenal mechi 197 pamoja na kucheza katika klabu za West Ham, Bolton, Bournemouth na AGF Aarhus za Denmark, huku pia akiichezea England michezo 34.

Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari juzi, Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, alikataa kuthibitisha kujiuzulu kwa Wilshere lakini akasema: "Amekuwa mzuri. Kila mtu anajua kuhusu kazi yake, kuhusu tabia yake na yeye ni mtu wa kipekee sana. Mahusiano yake na klabu ya soka ni ya kipekee.

# Ten Hag: Ferguson hatakiwi kuondoka

**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag, amekiri kuondolewa kwa ajira ya Sir Alex Ferguson ndani ya Manchester United "itaathiri" klabu hiyo, lakini akasisitiza kocha huyo wa zamani bado atakuwa tayari kutoa ushauri kwa wachezaji na wafanyakazi.

United wameamua kuondoa jukumu la Ferguson kama balozi, ikiwa ni sehemu ya hatua za kupunguza gharama.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 82 alikuwa akipokea kiasi cha paundi milioni mbili kwa mwaka, tangu ajiuzulu kama kocha mwaka 2013.

"Bila shaka ina athari kwetu, Sir Alex ni Manchester United," alisema Ten Hag akiwaambia waandishi wa habari siku ya Ijumaa.

"Aliijenga United hadi pale klabu ilipo sasa, inatuathiri. Lakini kwa upande mwingine pia tunajua na Sir Alex anajua na anataka kuiona United ikishinda, nina uhakika yuko tayari kwa kila ushauri na nitamhitaji kama tulivyomhitaji katika miaka miwili na nusu iliyopita nikiwa hapa."

Ferguson alifurahia mafanikio yasiyo na kifani akiwa Old Trafford, akishinda mataji 13 ya Ligi Kuu England na michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mara mbili katika kipindi cha miaka 27.

Anabakia kuwa kocha wa mwisho wa United kushinda taji hilo na tangu kuondoka kwake zaidi ya miaka 10 iliyopita, klabu hiyo imeshuka kutoka kileleni katika soka la Uingereza.

"Kwa sasa hatuwezi kufikia viwango alivyoweka Ferguson, lakini bado tulishinda makombe," alisema Ten Hag.

"Kumbuka, miaka sita kabla klabu hii haijashinda mataji kwa hivyo tunarudi.



# CHANA AAHIDI SERIKALI KUIBEBA KILI MARATHON

Na Mwandishi Wetu

MBIO za kimataifa za Kilimanjaro Marathon, zimezinduliwa rasmi kwenye Ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere na kuelezwa zitafanyika ifikapo Februari 23, mwakani.

**Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Pindi Chana, alitangaza wizara yake ipo tayari kukaa pamoja na waandaaji wa tukio hilo muhimu na kuona njia ambazo zitakuza utalii wa ndani na wa kimataifa.**

Chana alisema mbio za masafa marefu zimeonekana ni moja ya matukio makubwa zaidi ya michezo nchini, hivyo ni jukwaa zuri la kukuza utalii.

"Tunajivunia mbio za masafa marefu za Kilimanjaro Premium Lager, kwa sababu zimeonekana ni moja ya matukio makubwa ya kimataifa katika ukanda huu, kutokana na kuwaleta pamoja zaidi ya washiriki 12,000 na idadi sawa ya watazamaji kutoka zaidi ya nchi 56 na wote hawa ni watalii watarajiwa. Hii ni hatua kubwa sana," alisema Chana.

Aliongeza wizara kabla na baada ya tukio hilo, itatangaza vivutio vya utalii vya kutosha kupitia tukio hilio kubwa, ili kuhakikisha watu wengi zaidi wanafikiwa kadiri iwezekanavyo.

"Nawapongeza wadhamini wote wakiongozwa na Kilimanjaro Premium Lager (mdhamini mkuu) na Tigo (kilomita 21), wadhamini wa mezani (maji) ni Simba Cement, Benki ya CRDB, Maji ya Kilimanjaro, TotalEnergies, Kiwanda cha Sukari cha TPC. Wasambazaji rasmi ni GardaWorld Security, CMC Automobiles, Sal Salinero na watoa huduma maalumu - Kibo Palace na Keys. Bila nyinyi isingekuwa rahisi," Chana alisisitiza.

Waziri pia aliwataka washiriki na watazamaji kutumia msimu wa mbio za masafa marefu kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii, ikiwa ni pamoja na Mlima Kilimanjaro, Serengeti, Ngorongoro, Zanzibar na vivutio vingine.

Naye Mkurugenzi wa Masoko wa Kampuni ya Bia Tanzania (TBL), Khensani Mkhombo, alisema wanajivunia kudhamini tukio hilo kwa miaka 23 sasa na kuufanya kuwa moja ya udhamini mrefu zaidi nchini, huku akiongeza miaka yote wametiwa moyo na msaada wa utalii na utamaduni wa Watanzania.

Alitoa wito kwa washiriki kujiandikisha kwa wakati kupitia www.kilimanjaromarathon.com na kupitia TigoPesa.

Meneja Chapa wa Kampuni ya Tigo, Woinde Shisael, alisema wao wanaadhimisha miaka 30 ya kubadilisha maisha kupitia ubunifu wa kidijitali na kuadhimisha miaka 10 ya kujivunia kudhamini mbio za nusu marathoni.

"Tunatazamia mbio za kusisimua na muongo mwingine wa kuwawezesha Watanzania kupitia michezo na teknolojia," Shisaeli aliongeza.




Waziri wa Maliasili na Utalii Balozi Dk. Pindi Chana (wa tatu kulia) na Mkurugenzi wa Masoko wa Kampuni ya Bia Tanzania, Khensani Mkhombo (wa tatu kushoto) wakiongoza wageni wengine katika uzinduzi rasmi wa mbio za Kilimanjaro Marathon 2025 jijini, Dar es Salaam Ijumaa. Kulia ni Makamu wa Rais wa Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC), Henry Tandau. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ngorongoro Heroes yaipania Kenya

Na Somoe Ng'itu

TIMU ya Soka ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes), inakutana na Kenya katika mechi ya fainali ya michuano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-20) itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Ngorongoro Heroes ilitinga fainali hiyo baada ya kuifunga na kuwavua ubingwa Uganda mabao 2-1 wakati Kenya ilipa Rwanda kichapo cha magoli 4-0, katika mechi ya nusu fainali ya pili iliyochezwa juzi jioni.

Ngorongoro Heroes na Kenya rasmi zitaiwakilisha CECAFA katika Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON U-20), zitakazofanyika mwakani nchini Congo Brazzaville.

Kocha Mkuu wa Ngorongoro Heroes, Boniface Mkwasa, alisema wachezaji wake wako tayari na malengo yao yalikuwa ni kubeba ubingwa wa michuano ya mwaka huu.

Mkwasa alisema wako tayari kwa ajili ya mechi hiyo na wanaamini wataingia uwanjani kwa lengo la kulipa kisasi cha kufungwa na Kenya walipokutana hatua ya makundi.

"Tumefuzu ndio lilikuwa lengo kuu, lakini pia kutwaa ubingwa wa mashindano haya ni ndoto yetu, tumejiandaa kurekebisha makosa tuliyofanya tulipokutana katika mechi ya kwanza, tutaingia tofauti, tumeshawasoma wapinzani wetu," Mkwasa alisema.

Naye mshambuliaji wa timu hiyo, Jammy Simba, alisema wanatarajia kufuata maelekezo ya kocha wao, ili kupata ushindi na kuwafurahisha Watanzania.

"Hautakuwa mchezo rahisi, kila upande unahitaji kumaliza vyema michuano hii, lakini sisi pia hatutaki kuona tunafungwa mara ya pili na Kenya," Simba aliongeza.

## Azam FC kicheko kuifunga Prisons

Na Adam Fungamwango

AZAM FC imefurahi kuwa timu ya kwanza kuifunga Prisons nyumbani katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya, juzi, ambapo waliondoka na ushindi wa mabao 2-0.

Ofisa Habari wa Azam, Hasheem Ibwe, amesema timu yao imeondoa 'password' ya Prisons ambayo ilikuwa inajivunia kupitia mabao yaliyofungwa na Idd Selemani 'Nado' pamoja na Nassor Saaduni.

"Historia imeandikwa, msimu huu sisi Azam tumekuwa wa kwanza kuifunga Prisons nyumbani kwao, hongera kwa wachezaji wetu na kocha wetu pia," alisema Ibwe.

Naye Kocha Mkuu wa Azam FC, Rachid Taoussi, amesema haikuwa rahisi kupata ushindi huo wa ugenini.

"Haikuwa rahisi, sababu tumecheza vizuri kipindi cha kwanza, tulitawala mchezo halafu tukabadilisha uchezaji, kulia, kushoto, nyuma na tumefunga mabao mawili, tumefanya kama ambavyo huwa tunafanya kwenye mazoezi," Taoussi alisema.

## Bocco aingia vitani rasmi Ligi Kuu Bara

Na Adam Fungamwango

STRAIKA mkongwe nchini, John Bocco, ameingia rasmi katika mbio za kusaka kiatu cha dhahabu kwenye Ligi Kuu Bara msimu huu dhidi ya nyota vijana, akiwamo Stephanie Aziz Ki wa Yanga na Leonel Ateba wa Simba.

Bocco amefunga mabao mawili wakati JKT Tanzania ikipata ushindi wa magoli 4-2 dhidi ya Tabora United. Straika huyo wa zamani wa Azam FC na Simba, aliyefunga zaidi ya mabao 100 katika misimu 17 ya Ligi Kuu aliyocheza mpaka sasa, alifunga goli la kwanza na la pili ndani ya dakika tano, kwenye mechi huo uliopigwa juzi, Dar es Salaam.

Mara ya mwisho kwa mchezaji huyo kutwaa kiatu cha dhahabu, ilikuwa ni 2020/21 alipomaliza akiwa amepachika mabao 16 akiwa na Simba, akiwahi pia kutwaa tuzo hiyo alipofunga mabao 19 akiwa na Azam FC. Bocco, amejiunga na JKT Tanzania msimu huu, akitokea Simba ambako aliachwa msimu uliomalizika na kupewa timu ya vijana chini ya miaka 17, lakini baadaye akaibuka kwa maafande hao.

Mabao mengine katika mechi hiyo ya juzi yalifungwa na Edward Songo na kiungo mshambuliaji wa zamani wa Simba, Said Ndemla, huku yale ya Tabora United yakipachikwa na Offen Chikola pamoja na Yacouba Sogne.

# Michezo

Jumapili Oktoba 20, 2024

Nipashe




Lewandowski na mkataba Barca UKURASA 22

# Yanga SC moto uleule

## Bao la kujifunga lawapa ushindi wa nne mfululizo dhidi ya Mnyama...

**Na Adam Fungamwango**

BAO pekee la kujifunga la beki wa kulia wa Simba, Kelvin Kijili, liliifanya Yanga kuendeleza ubabe katika dabi ya nne mfululizo, tatu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Kijili aliyeingia kuchukua nafasi ya Kibu Denis, alikwamisha mwenyewe wavuni mpira dakika nne kabla ya mechi hiyo kumalizika, akiwa katika harakati za kuokoa mpira uliopigwa na Maxi Nzengeli.**

Kiungo huyo wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, aliupiga mpira wa pembeni uliotemwa na kipa wa Simba, Moussa Camara, aliyekuwa anapangua faulo ya Clatous Chama, ambaye naye aliingia kipindi hicho kuchukua nafasi ya Stephane Aziz Ki.

Alikuwa ni Augustine Okejepha aliyeingia kuchukua nafasi ya Yusuph Kagoma, aliyefanya madhambi nje kidogo ya hatari na kusababisha faulo iliyoenda kuzaa bao hilo, ambalo limewapa pointi tatu muhimu mabingwa hao watetezi.

Ushindi huo wa bao 1-0 katika mechi hiyo ya raundi ya nane ya Ligi Kuu iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, umeifanya Yanga kuifunga Simba kwa mara nyingine tena kwa kipindi kisichopungua miezi miwili, ushindi kama huo walipata katika mchezo wa Ngao ya Jamii uliochezwa Agosti 8, mwaka huu.

Msimu uliopita Yanga iliifunga Simba katika michezo yote ya mizunguko miwili, Novemba 5, mwaka jana iliwachapa mabao 5-1 na Aprili 20, mwaka huu ikashinda mabao 2-1.

Simba ndiyo walianza mchezo kwa kasi na ilionekana wanasaka bao la mapema, ikifanya mashambulizi makali dakika ya kwanza na ya tano. Yote walimhusisha straika wao tegemeo, Leonel Ateba, ambapo dakika ya kwanza tu aliunganisha kwa kichwa mpira wa faulo iliyopigwa na Jean Charles Ahoua, lakini uliwababatiza mabeki wa Yanga na kutoka nje, ikawa kona.

Dakika nne baadaye straika huyo raia wa Cameroon, alikosa bao la wazi alipobaki yeye na kipa wa Yanga, Djigui Diarra, lakini chenga aliyotaka kumpiga haikufanikiwa, badala yake nyota huyo raia wa Mali, alifanikiwa kuukoa mpira kwa mkono.

Kama vile haitoshi mpira aliookoa Diarra ulikwenda kwenye mguu wa kulia wa Joshua Mutale, ambaye alitandika shuti lililombabatiza kipa huyo na kuikoa Yanga.

Yanga ilifanya shambulio la kwanza langoni mwa Simba dakika ya 13, wakati krosi ya Shadrack Boka, ilikosewa kuokolewa na mabeki, nusura wajifunge kabla Camara hajautia mikononi.

Kuanzia wakati huo, Yanga ilionekana kutulia na kufanya mashambulizi kwenye lango la wapinzani wao, ambapo dakika ya 21, Camara alilazimika kutoka langoni na kupangua mpira wa krosi ya Yao Kouassi iliyokuwa inatua kichwani kwa Maxi bila kukabwa na beki yoyote wa Simba.

Jaribio lingine lilifanywa na Stephane Aziz Ki, dakika ya 27, alipomhadaa, Yusuph Kagoma na kupiga shuti kali la mguu wa kushoto, lililombabatiza beki wa Wekundu wa Msimbazi, Fondoh Che Malone na kumpoteza maboya kipa Camara, lakini ukatoka nje na kuwa kona tasa.

Faulo iliyopigwa na Ahoua dakika ya 37, ilitua kichwani na Abdulrazack Hamza, lakini hakulenga lango, badala yake mpira ulipaa juu la lango.

Yanga ilikaribia kufunga bao dakika tatu kabla ya kwenda mapumziko, baada ya wachezaji wa Simba kudhani mpira aliokuwa akiukokota, Pacome Zouzoua umetoka nje, wakati wakinyoosha mikono, alipiga krosi ya ndani iliyomkuta Aziz Ki akiwa katika nafasi nzuri kabla na kuachia shuti kali karibu na lango ambapo ulimkuta Camara yuko imara na aliudaka, ukamponyoka na kugonga nguzo ya pembeni kabla ya kuudhibiti tena usiingie wavuni.

Kipindi cha pili Yanga iliingia na kucheza na kasi tofauti na wapinzani wao ambao walikuwa wanapoozesha mpira, na iliwafanya kulishambulia lango la Simba mfululizo hadi walipofanikiwa kupata bao.

Mabadiliko ambayo iliyafanya kipindi cha pili cha kuwaingiza, Chama, Clement Mzize waliochukua nafasi ya Mzimbabwe Prince Dube na Kennedy Musonda aliyeingia kuchukua nafasi ya Pacome, yalionekana kuipa uhai na kuweza kuibuka na ushindi huo.

Matokeo ya mchezo huo yanaifanya Yanga kufikisha pointi 15 na kwenda mpaka nafasi ya pili ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, chini ya vinara Singida Black Stars yenye pointi 16, lakini imecheza mechi zaidi.

Mabingwa hao watetezi wameweka rekodi ya kucheza michezo mitano, ikishinda yote, ikifikisha mabao tisa bila kuruhusu wavu wake kuguswa na kuendelea kutopoteza mechi.

Kipigo ilichokipata Simba ni cha kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, ikishuka hadi nafasi ya nne kwenye msimamo ikisalia na pointi 13 kibindoni.



Kipa wa Yanga, Djigui Diarra (kulia), akiwania mpira dhidi ya mshambuliaji wa Simba, Leonel Ateba katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. Yanga ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >